HALIUZWI

# JARIDA LA MASHTAKA

## HAKI, AMANI NA USALAMA KWA MAENDELEO YA TAIFA

**Toleo Na. 2 Julai, 2023 - June, 2024**




Aliyekuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Dkt. Khatibu Kazungu (katikati) akizindua jengo la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Shinyanga ambalo linawakilisha uzinduzi wa majengo yote ya Ofisi za Mikoa yaliyojengwa na yanayoendelea kujengwa.

// BODI YA UHARIRI

| | |
|---|---|
| **Mwenyekiti** | Sylvester Anthony Mwakitalu<br>Mkurugenzi wa Mashtaka |
| **Makamu Mwenyekiti** | Bibiana Joseph Kileo<br>Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka |
| **Mhariri Mkuu** | Rebecca Philip Kwandu<br>Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini |

Faraja A. Nchimbi
Mkurugenzi Divisheni ya Utaifishaji Mali, Makosa Yanayovuka Mipaka na Uhalifu Mahsusi

Pendo E. Makondo
Mkurugenzi Msaidizi Sehemu ya Utenganishaji wa Shughuli za Mashtaka na Upelelezi

Zamaradi M. Kawawa
Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Habari Maelezo

Marygoreth L. Ntandu
Afisa Habari

Tawabu Issa
Wakili wa Serikali

Henry J. Mwakigali
Afisa TEHAMA

Msanifu wa Jarida: Afisa TEHAMA

# Tahariri ya Mhariri



## Rebecca P. Kwandu

### Mhariri Mkuu

Napenda kuchukua fursa hii kuwakaribisha wasomaji wetu wa Jarida la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kusoma Toleo la Pili la Jarida la Mashtaka ambalo hutoka mara mbili kwa mwaka.

Katika Toleo la Kwanza Jarida lililenga katika kuelimisha umma juu ya historia ya kuanzishwa kwa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Muundo wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuanzia ngazi ya Makao Makuu, Mkoa na Wilaya pamoja na Majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Toleo la Kwanza pia lilikuletea makala mbalimbali juu ya Ulinzi wa Mashahidi katika Mfumo wa Haki Jinai, Miongozo ya Maamuzi ya Kushtaki na Makala juu ya Dhamana katika Jinai. Jarida pia, lilikuletea utani wa kisheria na kukuhabarisha vidokezo vya mambo usiyoyajua (Je wajua?)

Ndani ya Toleo hili la Pili, Jarida linalenga kukuletea habari na makala maalum zenye lengo la kuelimisha umma juu ya majukumu na mambo mbalimbali ya msingi yaliyotekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kipindi cha miezi sita kuanzia mwezi Januari, 2024 hadi mwezi Juni, 2024.

Baadhi ya makala zilizopo kwenye jarida hili zinahusu uendeshaji wa mashauri ya wanyamapori, taratibu za mwenendo kabidhi (Committal Proceedings), usimamizi na utaifishaji wa mali zitokanazo na uhalifu, makosa yanayohusiana na picha za ngono za watoto (Child Ponography), matumizi ya ushahidi wa kisayansi katika uthibitishaji wa makosa ya jinai. Pia msomaji atapata nafasi ya kusoma makala kuhusu Mwongozo wa Uendeshaji wa kesi dhidi ya ukatili wa kijinsia.

Vilevile zipo picha na makala zinazoonesha namna Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inavyojihusisha na kufanya vyema katika michezo.

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inaendelea kutekeleza majukumu yake kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa haki jinai wakiwemo Mahakama, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Jeshi la Polisi na Jeshi la Magereza. Ushirikiano huo unalenga kuhakikisha kuwa haki, amani na usalama unapatikana katika jamii yetu. Hili limefanyika kwa kushirikiana na wadau pamoja na mambo mengine, kufanya vikao vya haki jinai katika ngazi ya kitaifa, mkoa na wilaya. Vikao hivyo vina lengo la kujadili masuala mbalimbali yanayohusu uendeshaji wa kesi za jinai pamoja na kuratibu upelelezi kwa lengo la kuhakikisha haki inapatikana kwa wakati.

Jarida litaainisha baadhi ya matukio muhimu yanayobainisha ushirikiano baina ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na wadau wa haki jinai katika kutekeleza majukumu yake.



# NENO KUTOKA KWA MWENYEKITI WA BODI YA UHARIRI

**Sylvester Anthony Mwakitalu**
**Mkurugenzi wa Mashtaka**

Toleo la pili la Jarida la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka linalenga kuelimisha umma juu ya majukumu na mambo mbalimbali ya msingi yaliyotekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kipindi cha miezi sita kuanzia mwezi Januari, 2024 hadi mwezi Juni, 2024.

Katika kipindi cha miezi sita Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imekuwa ikitekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuhakikisha kuwa inashughulikia mashauri yote ya Jinai kwa ueledi. Toleo la Pili la Jarida la Mashtaka litamwezesha msomaji kujifunza mambo mbalimbali yanayohusiana na utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka inayoongozwa na Dira ya Haki, Amani na Usalama kwa maendeleo ya Taifa letu na dhima inayolenga kushirikiana na wadau kuendesha kesi za jinai bila woga, upendeleo au ubaguzi na kuhakikisha Haki, Amani na Usalama vinatamalaki katika jamii.

Jarida limewaletea pia, miongoni mwa kesi mashuhuri zilizoweka misimamo ya kisheria, mfano kesi ya Waziri Amani dhidi ya Jamhuri ambayo ilitolewa maamuzi na Mahakama ya Rufani zaidi ya miaka 44 iliyopita na kuweka kanuni ya utambuzi wa mshtakiwa katika eneo la tukio na kesi ya Yanga Omari dhidi ya Jamhuri ambapo mtuhumiwa ni mfanyabiashara wa dawa za kulevya ambayo imedhihirisha kuwa uhalifu haulipi.

Kipaumbele cha Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ni kuimarisha mapambano dhidi ya uhalifu kwa lengo la kuwafanya wahalifu na jamii kwa ujumla watambue kuwa uhalifu haulipi ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kuzingatia majukumu ya Ofisi hii ya kuhakikisha Haki inapatikana katika jamii, toleo hili litajumuisha matukio muhimu yaliyofanywa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuanzia mwezi Januari, 2024 hadi Juni, 2024. Pamoja na Makala hizo utajionea picha za matukio mbalimbali za shughuli zilizotekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Napenda kuchukua nafasi hii kuishukuru Bodi ya Uhariri wa jarida pamoja na Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa kufanya kazi kama timu na kuwezesha kupatikana kwa matokeo makubwa.

Nachukua fursa hii kuwasihi wasomaji kusoma jarida hili ili kuongeza ufahamu juu ya shughuli mbalimbali zinazotekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

# KONA YA NAIBU MKURUGENZI WA MASHTAKA



**Bibiana Joseph Kileo**
**Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka**

Msomaji wa Jarida la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka karibu ujumuike nasi kusoma Habari na Makala mbalimbali ambazo Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imekuletea kwa lengo la kuelimisha na kukufahamisha juu ya utekelezaji wa majukumu mbalimbali yaliyotekelezwa katika kipindi cha miezi sita kuanzia mwezi Januari, 2024 hadi Juni, 2024.

Katika kipindi cha Miezi Sita Ofisi ya Taifa ya mashtaka imeendelea kutekeleza majukumu yake mbalimbali yakiwepo majukumu ya uendeshaji wa kesi za jinai katika mahakama zote isipokuwa za kijeshi, uratibu na usimamizi wa shughuli za upelelezi, ushughulikiaji wa majalada kutoka vyombo vya upelelezi, ukaguzi wa magereza na vituo vya polisi, ushirikiano na wadau wengine wa haki jinai pamoja na utekelezaji wa programu ya utenganishaji wa shughuli za mashtaka na upelelezi.

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeweza kutekeleza majukumu hayo kwa ufanisi na kupata mafanikio ikiwemo kupunguza mlundikano wa kesi katika Mahakama za Wilaya, Mahakama za Hakimu Mkazi, Mahakama Kuu na Mahakama za Rufani na kuwezesha kupunguzwa kwa msongamano wa mahabusi katika magereza nchini.

Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imefanikiwa kusogeza huduma kwa jamii kwa kufungua Ofisi za Mashtaka katika Wilaya 92 nchini na kuwezesha kupungua kwa malalamiko kwa Serikali pamoja na kuwezesha kuokoa Mali za Serikali.

Ushirikiano uliopo kati ya Menejimenti, watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na wadau mbalimbali wa haki jinai ndiyo nguzo kuu iliyotuwezesha kutekeleza majukumu yetu kwa ufanisi.

Nidhamu kwa watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na kujituma katika utekelezaji wa majukumu yao vimeongeza tija katika utendaji kazi. Napenda kutumia fursa hii kuwashukuru Menejimenti na watumishi kwa ushirikiano mkubwa wanaotoa katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

Nawakaribisha kusoma jarida hili ili muweze kujihabarisha juu ya mambo mbalimbali yanayotekelezwa na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka.

# Yaliyomo


Uk. 07 Ofisi ya Taifa Mashtaka Yapata Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka

Uk. 09 Uendeshaji wa Mashauri Mahakamani Kwa Mfumo wa Kificho "Sheria Uzoefu"

Uk. 13 Ni Namna Gani Watoto Wanakumbwa na Janga la Ponografia

Uk. 16 Matumizi ya Ushahidi wa Kisayansi katika Kuthibitisha Makosa ya Jinai: Changamoto na Matarajio

Uk. 24 Habari Picha

Uk. 26 Miaka Arobaini na Nne (44) ya Kesi ya Waziri Amani

Uk. 27 Mathias Bundala na Sakata la Kumuua Mke Wake Mdogo Kwa Wivu wa Mapenzi

Uk. 29 Uendeshaji wa Mashauri ya Wanyama Pori: Uombaji na Utolewaji wa Amri za Uteketezaji wa Nyara Zinazoharibika Kwa Haraka

Uk. 32 Uhalifu Haulipi

Uk. 36 Mashtaka Sports yatikisa katika michezo ya SHIMIWI na MEI MOSI

Uk. 38 Msiba wa Joseph Sebastian Pande Aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Uliogeuka Kuwa Darasa la Uongozi na Utu

Uk. 41 Utani wa Kisheria



*Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan akimuapisha Bi. Bibiana Joseph Kileo kuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka katika hafla fupi iliyofanyika tarehe 28 Aprili, 2024 Jijini Dar es salaam*

# Ofisi ya Taifa Mashtaka Yapata Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan tarehe 28 Aprili, 2024 alimwapisha Bi. Bibiana Jeseph Kileo kuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka baada ya kumteua kuziba pengo la marehemu Joseph Sebastian Pande. Kabla ya uteuzi huo Bi. Bibiana Joseph Kileo alikuwa Mkuu wa Mashtaka mkoa wa Mwanza.

Baada ya kuapishwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana alikutana na watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Jijini Dar es Salaam na Dodoma Makao Makuu ambao walimpokea na kuzungumza nao baada ya mapokezi akiwa ameongozana na Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu ambapo aliwataka watumishi kufanya kazi kwa kuzingatia haki, upendo na ushirikiano kwa lengo la kusukuma gurudumu la maendeleo ya jamii na taifa kwa ujumla.

"Namshukuru sana Rais wa Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa kuniamini na kuniteua kuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, ninaahidi kujitahidi kwa uwezo wangu wote kusaidia majukumu yako kwa weledi na uadilifu mkubwa." Alisema Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bibiana.

Akizungumza katika kikao hicho cha mapokezi kilichofanyika katika ukumbi wa Makao Makuu ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka jijini Dodoma Bi. Kileo alisema Ofisi ina jukumu la kikatiba chini ya Ibara 59B ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya kusimamia uendeshaji wa mashtaka nchini ambapo alieleza kuwa jukumu hili linapaswa kufanyika kwa kuzingatia misingi ya haki na maslahi mapana ya nchi.

“Ofisi yetu imepewa jukumu kubwa la kuamua juu ya hatma za watu, hivyo watumishi wa ofisi hii wanapaswa kufanya kazi kwa weledi mkubwa, kuzingatia sheria na bila kuwa na upendeleo wala kumwonea mtu. Alisema Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka.

"Ninaomba tushirikiane pamoja katika kutimiza jukumu hili ili kuifanya taasisi yetu kuwa bora na inayoongoza kwa kutenda haki ndani ya nchi hii." Alieleza Naibu Mkurugenzi Bibiana.

Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka pia alitumia fursa hiyo kutoa pongezi kwa menejimenti kwa ushirikiano wanaoutoa kwa watumishi kwa kupambana usiku na mchana na kuifanya taasisi izidi kusonga mbele ili kuwawezesha wananchi kupokea huduma wanazostahili kutoka kwao na kuwezesha kupungua kwa malalamiko kutoka kwa wananchi na kesi kusikilizwa kwa wakati.



*Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana Kileo akipokea ua la ukaribisho kutoka kwa Afisa Utumishi Bi. Rahel Sirari mara baada ya kuwasili Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Makao Makuu Jijini Dodoma katika hafla fupi ya Ukaribisho iliyofanyika tarehe 30 Aprili, 2024.*

# UENDESHAJI WA MASHAURI MAHAKAMANI KWA MFUMO WA KIFICHO "SHERIA UZOEFU"

**Na Renatus Mathias Mkude**

**Mkurugenzi Msaidizi Ofisi ya Taifa ya Mashtaka anayehusika na makosa dhidi ya Binadamu na Utangamano wa Taifa.**

## 1. UTANGULIZI

Uendeshaji wa mashauri mahakamani nchini Tanzania imekuwa ni sehemu ya Utoaji haki kwa kipindi chote kabla na baada ya Uhuru. Mifumo yote ya madai na jinai wananchi wameitumia ili kupata haki wanazostahili. Kwa upande wa sheria za jinai, miendendo yake inafuata taratibu mbalimbali zilizowekwa kisheria ambazo hufuata taratibu za ndani ya nchi na nchi ambazo tumeridhi mifumo yake ya kisheria na miendendo hii ya uendeshaji mashauri hutumia vyombo mbalimbali ikiwemo vyombo chunguzi, taasisi ya mashtaka, mahakama na taasisi za marekebisho kama Magereza. Usikilizaji wa mashauri kimsingi ni kanuni ya ujumla kuwa yanapaswa kusikilizwa katika mahakama ya wazi ili watu wote na jamii washuhudie kama vile msemo maarufu wa kisheria unaosema kuwa "haki haipaswi tu kutendeka bali kuonekana inatendeka".[1]

Mfumo huu unatumika katika nchi nyingi duniani isipokuwa kwa baadhi tu ya mashauri ambayo ili kulinda utu wa mtu na makundi maalumu au usalama wa nchi basi sheria za nchi husika au maamuzi ya mahakama hutaka aina fulani ya mashauri kusikilizwa kwa kificho maarufu kwa lugha ya kiingereza kama "proceedings in camera". Makala hii itaangalia utaratibu unavyotumika duniani na hapa Tanzania kwa kuangalia sheria mbalimbali na uzoefu wa mazoea ya kimahakama. Tutaona kwa ujumla uelewa wanajamii na wanasheria na hatimaye faida na changamoto zake na kupendekeza maboresho husika.

## 2. NINI MAANA YA USIKILIZWAJI WA MASHAURI KWA KIFICHO

Usikilizwaji wa mashauri mahakamani kwa kificho ni utaratibu unaotumiwa na mahakama katika kusiliza aina fulani ya mashuri yanayohusisha makosa fulani au aina fulani ya watu bila kuruhusu watu wengine tofauti na wahusika katika shauri kuhudhuria au vyombo vya habari kwa lengo la kutotoa taarifa fulani kutokana na unyeti wake. Katika mashauri ya jinai Hakimu au Jaji anaweza akasikiliza shauri kwa kificho mwanzo mpaka mwisho au sehemu ya mwenendo ili kusoma au kupokea sehemu fulani ya ushahidi ikiwemo taarifa nyeti au fichi au kuendesha usuluishi baina ya wadaiwa wa shauri. [2]

## 3. TAFSIRI ZISIZO ZA KISHERIA

Usikilizaji mashauri kwa kificho inaweza kuwa vikao au mashauri nyeti ya kampuni yanayohusu masuala nyeti kama ya mtumishi ,fedha, mbinu za biahara za ndani ya kampuni na hivyo kutoruhusu mtu au watu

1 *Lord Hewart, aliyewai kuwa Jaji Mkuu wa Uingereza akiwa katika shauri la Rex v. Sussex Justices, [1924] 1 KB 256".*

2 *Wex definition team, Cornel Law School, Legal Information Institute 2023. Angalia pia United States v. Zolin, 491 USA 554 (1989) na ONESMO LAURENT @ SALIKOKI versus R, Criminal Appeal 458 of 2018 CAT, Moshi.*

wengine kuhudhuria.

## 4. HISTORIA FUPI YA MFUMO WA USILIZAJI MASHAURI KWA NJIA YA KIFICHO.

Utaratibu wa usikilizwaji wa mashauri kwa kificho umeanza siku nyingi nchi mbalimbali haswa Uingereza, Marekani na India na uliohusishwa sana na wanaharakati wa haki za binadamu waliotaka kulinda utu wa watu. Baadae wakati mabadiliko ya mifumo ya kisheria inaendelea uendeshaji mashauri kwa kificho umekuwa kama sehemu ya ulinzi wa mashahidi haswa wahanga wa matukio. Kwa kiasi ulilenga kuficha baadhi ya taarifa kutojulikana na umma na ndio maana vyombo vya habari na wanahabari hawakuruhusiwa kuchukua habari na kupeleka kwa umma.

Kimsingi chimbuko la usikiliwa mashauri kwa kificho au faragha lilipata nguvu kutokana na uwepo wa mikataba ya Kimataifa,[3] kikanda[4] na katiba za nchi ambazo kwa pamoja zimetamka misingi ya kulinda hakai za binadamu ikiwemo haki ya ulinzi, utu, kusikilizwa kwa bila uonevu na haki za ujumla.Misingi katika mikataba hiyo ilipelekea kutungwa kwa mikataba mingine ya makundi maalumu kama wanawake na watoto ambavyo inaendeleza misingi hiyo mikuu.

## 5. USIKILIZAJI WA MASHAURI KWA KIFICHO NCHINI TANZANIA

Kwa upande wa Tanzania Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeweka haki ya kulindwa na usawa mbele ya sheria na wakati wote kuzingatiwa utu wa mtu.[5] Kwa upande wa Tanzania kanuni ya ujumla ni kuwa mashauri yote yanapaswa kusikilizwa katika mahakama za wazi na ikibidi kuwepo vyombo vya habari.[6] Hata hivyo sheria imeweka utaratibu wa kusikiliza baadhi ya mashauri ya kiutawala na kimahakama kwa mfumo wa kificho. Hii ni pamoja na mashauri yanayohusu makosa ya kujamiana[7], utolewaji wa ushahidi wa mhanga wa usafirisaji haramu wa binadamu,[8] mashauri katika mahakama za watoto,[9] mashauri katika Kamati ya Maadili ya Mawakili,[10] mashauri katika Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Umma[11], Mashauri ya nidhamu za kitaaluma katika Taasisi za kitaalum, mashauri katika mahakama za kijeshi[12] na mengine ambayo yana mifumo ya tarifa za siri. Katika mahakama za kawaida kuna takwa la kufanya maombi maalumu ili mahakama kutoa amri ya shauri kusikilizwa kwa kificho na mashauri mengine sheria imetamka kufaya hivyo.[13]

## 6. SHERIA NA KANUNI ZINAZOSIMAMIA USIKILIZAJI WA MASHAURI KWA KIFICHO.

Kimsingi usikilizwaji wa mashauri kwa kificho una chimbuko katika sheria mbalimbali lakini zinazotumika mara nyingi ni ikiwemo Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania,[14] Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20,[15] Sheria ya Ushahidi Sura ya 6,[16]Sheria ya Ugaidi,[17] Sheria ya Mahakimu,[18] Sheria ya Mtoto,[19] . Zipo Kanuni na miongozo mbalimbali ikiwemo Mwongozo wa Jaji Mkuu wa Uendeshaji wa mashauri ya Watoto,[20] Miongozo ya Mkurugenzi wa Mashtaka ikiwemo Mwongozo wa Mkurugenzi wa Mashtaka kuhusu

---

3 *Ibara ya 2(2), (3b), 10(1)(3) na 14(4) ya Mkataba wa Kimataifa wa Haki za Kisiasa na Kiraia, 1966*
4 *Ibara ya 3, 4 na 5 ya Mkata wa Afrika wa Haki za Binadamu na Watu.*
5 *Ibara ya 12(2) na 13 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977*
6 *Section or case law*
7 *Kifungu cha 186 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai Sura ya 20,*
8 *Kifungu cha 4 Sheria dhidi ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu.*
9 *Kifungu cha 8 na 11 cha Sheria ya Mtoto Kanuni za Taratibu za Mwenendo Mahakamani 2016 ambayo ni GN 182/2016.*
10 *Kifungu cha 23 cha Sheria ya Mawakili wa Kujitegemea.*
11 *Kifungu cha Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake.*
12 *Kifungu cha 73 cha Sheria ya Ulinzi ya Tanzania.*
13 *Mfano Kifungu cha 186 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai tajwa hapo juu. Angalia pia Mkurugenzi wa Mashtaka dhidi ya Abdi Sharif Hassan@ Msomali na Wenzake, shauri la Maombi namba 19/2020 Mahakama Kuu Mwanza.*
14 *Ibara ya 12 na 13*
15 *Kifungu cha 186*
16 *Kifungu cha*
17 *Kifungu cha*
18 *Kifungu cha 14(1)(2)*
19 *Kifungu cha 97. Pia angalia Stephen Mbemba dhidi Hassan Maulid, shauri la mapitio namba 2 la 2019 Mhakama Kuu Dodoma*
20 *Kifungu cha 7 na 8*

Upelelezi na Ushughulikiaji wa mashauri ya Ubakaji,[21] na miongozo na Kanuni zingine. Yapo pia maamuzi mbalimbali ya mahakama kuhusu usikilizaji wa mashauri kwa kificho.[22]

## 7. TAASISI HUSIKA KATIKA USIKILIZAJI WA MASHAURI KWA KIFICHO

Kwa mujibu wa sheria zipo Taasisi kadhaa zinazohusika katika mnyororo wa kushughulika na usikilizwaji wa mashauri kwa faragha lakini kwaa minajili ya Makala hii inayogusa masuala ya kijinai ni zile taasisi ambazo zinahusika na hatua hizo za mnyororo wa haki jinai kuanzia ukamati, mashtaka, usikilizaji na urekebishaji. Mahakama ndio msimamizi mkuu wa utaratibu husika akifatiwa na wadau wake kama OTM,Polisi Idara ya Ustawi wa Jamii magereza n.k

Mtu anaweza kujiuliza kuwa ni kwa nini baadhi ya mashauri sheria imeweka utaratibu yasilizwe kwa faragha kama vile yale ya makosa ya kujamiana. Ni wazi kuwa utu na heshima ni tunu ambayo kila binadamu anaipenda na kuitaka na haswa ile ya kutoka katika jamii nzima. Kwa mfano nchi zingine kama India suala hili limewekwa katika katiba ikiwemo mashauri yanayohusu ndoa,taraka,uzinifu na usalama wa taifa.[23] Suala hili lilitiliwa mkazo na Jaji Bachawat wa India.[24] Lengo kubwa kushirikisha wahusika tu shauri kuhudhuria shauri ni pamoja na kuwapa nafasi ya kuwa huru kujieleza na kulinda baadhi ya taarifa zao binafsi kutokwenda kwa umma na zaidi kulinda taarifa fiche za kitaifa.[25]

## 8. MAMBO YA KUJIFUNZA KUTOKA NCHI ZINGINE.

Kama ilivyoelezwa hapo juu mfumo huu ni wa kihistoria na ulianza kwa misingi ya kulinda haki za binadamu na mfano zipo nchi nyingi zina uzoefu mkubwa kama vile Uingereza,Marekani na India iliyotajwa hapo juu na hata nchi za Afrika ikiwemo Kenya. Hata katika nchi hizo chimbuko ilikuwa ni sehemu ya ulinzi wa mashahidi katika mifumo ya Haki. Katika kuangalia mifano michache Katika nchi ya Uingereza imeweka njia kadhaa za ulinzi wa mashahidi kulingana na mazingira ya mashauri husika ikiwemo kusikiliza kwa kificho.[26] Mfumo wa ulinzi wa mashahidi wa 2018 wa sheria ya India umeweka mfumo wa ulinzi ikiwemo kusikiliza mashauri kwa kificho na umelindwa na katiba ya nchi hiyo.[27] Nchi ya Kenya imeweka utaratibu wa ulinzi wa mashahidi ikiwemo kusikiliza mashauri kwa mfumo wa kificho na kuanzisha taasisi maamlumu ya ulinzi wa mashahidi.[28]

Hata katika mahakama za kimataifa zina mifumo thabiti ya kulinda mashahidi ikiwemo kusikiliza mashauri kwa kificho. Mfano Mahakama ya Kimataifa ya Jinai kwa kutambua umuhimu wa mfumo huu ina mifumo ya kusiliza mashauri kwa kificho.[29]

## 9. FAIDA NA CHANGAMOTO ZA USIKILIZAJI WA MASHAURI KWA KIFICHO

Siku za karibuni kumekuwa na mjadala kuhusu uwepo wa usikilizaji mashauri kwa kificho haswa katika zama za uwazi na ukweli na kukuwa kwa teknolojia ambapo mahakama nyingi usikilizaji mashauri ufanyika kwa mtandao. Suala hili limeleta mjadala kuhusu utaratibu huu na hivyo kuona umuhimu wa kujadili faida na changamoto zake.

### 9.1 Faida za mfumo

9.1.1 Inazuia watu kuanza kujadili hukumu kabla ya wakati.

*21 Kifungu cha 4.5.2(a)*
*22 Stephen Mbemba hapo juu.*
*23 Ibara ya 21 ya Katiba ya India*
*24 Naresh vs. State of Maharastra (AIR 1967 SC 1)*
*25 Kanubhai vs. Meena*
*26 Sheria ya Haki za Vijana na Sheria Ushahidi ya 1999.*
*27 Ibara ya 21 ya Katiba ya India.*
*28 Ibara ya 50(8) na (9) ya Katiba ya Kenya na Sheria ya Ulinzi wa Mashahidi ya Sura ya 79. Rejea pia shauri la Mahakama Kuu Meru, katika Jamhuri dhidi ya Doyo Galgalo wenzake 3 shauri la Jinai namba.16 la 2019*
*29 ibara ya 64(2) na (6)(e) wa Mkataba wa Mahakama ya Kimataifa na kanuni za uendeshaji wa mashauri. Angalia pia The Prosecutor vs William Samoei Ruto and Joshua Arab Sang, ICC-01/09-01/11*

9.1.2 Inalinda utu wa wahusika na haswa wahanga.
9.1.3 Kulinda usalama wa siri za nchi.
9.1.4 Uhakika wa ulinzi wa mashahidi.
9.1.5 Kuepuka uwezekano wa kurubuni mashahidi.

**9.2 Changamoto za mfumo**

9.2.1 Kuna uwezekano wa kuzuia uwazi kwa umma.
9.2.2 Inazuia na kubana wanazuoni wa sheria kujifunza maana wanahudhuria wale tu wanaohusika na mashauri hayo.
9.2.3 Inazuia pia jamii kwa mapana yake kupata nafasi ya kujifunza kama ilivyo malengo ya mahakama za wazi.
9.2.4 Watu walio mbali na majengo ya mahakama kukosa fursa ya kufatilia haswa wakati huu baada ya kukuwa kwa teknolojia
9.2.5 Washtakiwa na wadau kukosa nafasi ya kujua ushahidi mapema haswa kwa Mahakama Kuu yenye mfumo wa upande wa mashtaka kuonesha ushahidi kabla ya kusikiliza.[30]

## 10. HITIMISHO.

Kutokana na maboresho ya mifumo ya haki jinai duniani na ili kuweka ulinganifu wa pande zote za mashauri mahakamani suala la ulinzi wa mashaidi halikwepeki. Usikilizwaji wa mashauri kwa faragha kwa baadhi ya mashauri ni hatua muhimu katika mifumo hiyo ili kulinda haki na utu wa watu na kuwafanya kuwa huru. Tanzania iendelee kutumia uzoefu wa nchi zingine zilizofanya vizuri kwa malengo ya maboresho ya mifumo ya haki jinai kwa maslai mapana ya taifa na haswa haki jinai.Hata hivyo changamoto zilizoainishwa zifanyiwe kazi na mamlaka ili kuleta tija na haswa mapendekezo yaliyoanishwa katika Tume ya Mheshimiwa Rais ya Maboresho ya Haki Jinai.[31] Bado mfumo wa usikilizwaji wa mashauri kwa kificho ni dhana nzuri katika hutoaji haki na hivyo wadau wote ikiwemo wapelelezi, waendesha mashtaka,Mahakimu na Majaji na wadau wengine washirikiane na kuendelea kutumia nyenzo hii katika kutenda haki.

30 *Kifungu cha 245-246 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai.*
31 *Rejea Taarifa fupi ya Tume ya Rais ya Maboresho ya Taasisi za haki jinai, 2023.*

# Ni Namna Gani Watoto Wanakumbwa na Janga la Ponografia

**Na Tulumanywa Majigo**
**Wakili wa Serikali**

## UTANGULIZI

Jaji Dlodlo D. V wa Mahakama ya Juu ya Rufani (The Supreme Court of Appeal) Afrika Kusini katika shauri la Essop v State[1], anaeleza madhara ya ponografia kwa watoto kuwa yanaathiri heshima na mwenendo wa makuzi ya mtoto. Kauli hii inasadifu athari za ponografia katika mazingira yetu, kwani vipo visa vingi vibaya ambavyo vimeathiri watoto kutokana na kutazama au kujihusisha na ponografia. Visa vya ponografia kuvitaja kwa uchache hapa nchini, vipo vingi vya matukio ya ulawiti yalivyosheheni maeneo mbalimbali ikiwemo mashuleni, majumbani na vituo vya kulelea watoto nakadharika.

Hivi karibuni imetokea katika darasa moja ambapo ilielezwa kuwa wanafunzi wa kiume wa darasa la nne katika Shule ya Msingi hapa nchini (jina limehifadhiwa) walikuwa wakiingiliana kinyume na maumbile. Chanzo kilibainika kwamba kilitokana na Mwanafunzi mmoja ambaye alitazama ponografia za watu waliokuwa wanaingiliana kinyume na maumbile katika mabanda umiza (maeneo maalumu ambayo watu hukusanyika na kulipia huduma ya kuangalia michezo mbalimbali ikiwemo mpira wa miguu kwa njia ya televisheni) naye akaona kama ni mchezo wa kawaida hivyo kwenda kuwafundisha wenzake shuleni na watoto wengine aliokuwa akicheza nao.

Kisa hiki kinatufundisha kuwa athari za mtoto anaye athirika na ponografia huathiri watoto wenzake maana mtoto haishi katika kisiwa hivyo mtoto mmoja anapoathirika na ponografia ni jamii nzima inakuwa imeathirika. Vilevile wazazi au walezi huathirika kwa kiwango kikubwa kwa kupoteza matumaini baada ya kubaini mtoto wao haendi katika makuzi mazuri kwa kuathirika na ponografia.

## MSINGI YA KISHERIA

Kutokana na madhara makubwa ya ponografia kwa watoto vita dhidi ya ponografia kwa watoto zimechukua sura ya Kimataifa na Kitaifa. Kimataifa ipo mikataba ya mbalimbali inayozitaka nchi washiriki kuweka mikakati ya dhati ya kupambana ponografia, mfano; Mkataba wa kimataifa kuhusu haki za watoto (International Convention on Rigth of the Child, 1990).

Kitaifa, kimsingi kila nchi imeweka utaratibu wa kupambana na ponografia mathalani Mwaka 2022, Uingereza iliandaa muswada wa kuimarisha ulinzi katika mitandao (The Online Safety Bill) ambapo muswada huo ulisaniwa na kuanza kama sheria kuanzia mwezi Oktoba 2023 ijulikanayo Sheria ya Usalama Mtandaoni (The Online Safety Act)[2], sheria hii imeweka takwa la watoa huduma za mtandao (Service Providers) kwa

1 *Case No.432/2020) [2021] ZASCA 66 (1 June, 2021*

2 *2023 Chapter 50 muswada ulipitishwa kuwa sheria tarehe 26 October, 2023.*

vigezo kuzuia watoto kutazama maudhui ya ponografia kwa kuweka vigezo vya kuchunguza umri wa mtoto kama vile kutumia matumizi ya vitambulisho na kuchukua jitihada mbalimbali kuweza kubaini umri wa mtoto kabla ya kutazama maudhui yanayohusiana na ponografia.

Sheria hiyo pia imeweka takwa la wazazi, walezi na watoto kutoa taarifa za uhalifu unao uhusiana na maudhui ya picha za unyanyasaji wa watoto mitandaoni. Kimsingi Sheria mpya ya Usalama wa Mitandao (The Online Safety Act) ya Uingereza imezingatia kumlinda mtoto katika kuzuia , Kukamata, Kupeleleza na Kushtaki uhalifu unaohusiana na ponografia.

Marekani kwa upande wake, pia iko mbioni kutunga sheria ya Usalama wa Watoto Mtandano (Kids Online Safety Act) kupitia muswada ulioandaliwa wa kuimarisha ulinzi katika mitandao (A Bill to Protect the Safety of Children on the Internet) ambapo muswada huo uliwasilishwa na kusomwa mara mbili kupitia wawakilishi wawili wa wananchi ambao ni Mr. Blumenthal na Bi. Blackburn katika Seneti na Baraza la Wawakilishi (Senate and House of Representatives) na sasa inafanyiwa kazi na Kamati[3], Mswada huu hii imeweka takwa la watumiaji wa vifaa vya umeme hasa vilivyounganishwa kwenye mtandao wakiwemo wazazi kuzingatia maslahi ya mtoto, kutowaumiza watoto na kujenga misingi ya ulinzi kwa watoto kutazama maudhui ya ponografia hasa wale wa miaka 16 au chini yake.

Kenya, kupitia sheria inayozuia matumizi mabaya ya kompyuta na makosa mtandao (The Computer Misuse and Cybercrimes Act, 2018) ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kujihusisha na ponografia ya watoto ikiwemo kuchapisha kwenye mtandao. Hivi karibuni Mahakama ya Watoto ya Milimani Nchni Kenya katika Shauri la jinai, kati ya Jamhuri dhidi ya Sharo Nanjala Wabwile alia Roshabavacanema Cherop[4], ukurasa wa 5 na 6 Mahakama kabla ya kutoa adhabu kwa mshitakiwa, ilijiuliza swali kwa nini mtoto analindwa kutokana na mwingiliano wa kimtandao?. Hivyo kwa kuzingatia sheria mablimbali Mahakama ilijiridhisha kwamba mtoto yupo katika makundi yenye mazingira magumu (vulnerable groups) na jukumu la ulinzi lipo kwa kila mmoja ili kuhakikisha kuwa wanatimiza malengo yao.

Hapa Tanzania, kifungu cha 13 na 14 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2015 ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kujihusisha na ponografia za aina yoyote ile ikiwemo za watoto kwa kuchapisha au kusababisha kuchapishwa au kutoa au kuweza upatikanaji kupitia katika mfumo wa kompyuta picha za ponografia au ponografia za watoto.

Ni namna gani Watoto wanakuwa wahanga wa Ponografia?

Mwanazuoni Sarah Skye Napier[5], katika Tasnifu yake ya Uzamivu anaeleza visa vingi ambapo watoto wanakuwa wahanga wa ponografia. Na kimsingi chanzo kikubwa cha athari za ponografia kwa watoto ni usimamizi usioridhisha wa matumizi ya mitandao kwa watoto. Hili lina uhalisia katika mazingira yetu kwani kwasasa si ajabu kumuona mzazi au mlezi anamwachia simu mtoto/kompyuta ambaye huitumia mitandao na kutazama maudhui yoyote atakayo pasipo usimamizi wa karibu. Ambapo imethibitishwa kuwa mbali ya watoto kuathirika na maudhui ya ponografia kupitia mitandao watoto wamekuwa wakirubuniwa na kufundishwa maadili/uhalifu na wahalifu kupitia mitandao pasipo wazazi/walezi kujua. Pia imeelezwa

3 *Kikao cha kwanza katika Mkutano wa Bunge 117.*

4 *Shauri la Jinai Na. E007/2024- natambua kuwa shauri hili lilisikilizwa na Mahakama ya Hakimu Mkazi Kenya, ambayo siyo mahakama ya kumbukumbu kisheria (court of record) lakini kutokana ukubwa ukubwa na madhara ya ponografia kwa watoto hivi sasa, ni vema kurejea uamuzi huu kwa ajili ya kubaini ukubwa wa tatizo na kuweka njia sahihi za utatuzi.*

5 *https://ses.library.usyd.edu.au/browse?type=author&value=Napier%2C+Sarah+Skye*

kuwa wazazi au walezi huwaruhusu watoto wao kutumia kompyuta kwa lengo la kucheza michezo mbalimbali bila kujua kwamba baadhi ya michezo hiyo imekuwa na maudhui ya kiponografia ambayo baadae huaribu makuzi na mwenendo wa Mtoto.

## HITIMISHO

Maudhui ya ponografia kwa watoto yanaangamiza Taifa la kesho, hivyo basi ili kuliokoa Taifa la kesho katika zama hizi za utandawazi ni pamoja na kuimarisha usimanizi kwa watoto katika matumizi ya mitandao. Suala la udhibiti wa ponografia haliwezi kufanikiwa ikiwa jukumu hili litaachiwa vyombo vya dola pekee pasipo ushiriki wa umma. Hivyo elimu ya kuhusiana na maudhui ya ponografia yanatakiwa kufahamishwa kwa umma ili kuwezesha kila mwananchi kuchukua hatua katika kudhibiti athari za ponografia kwa watoto.

Aidha vita dhidi ya athari za maudhui ya ponografia zitafanikiwa endapo kama kutakuwepo na hatua mahususi katika kuzuia kama vile utolewaji wa elimu kuanzia serikali za mitaa, mashuleni, nyumba za ibada, semina na mikusanyiko mbalimbali, kuwawajibisha watoa huduma za mitandao (Service providers), udhibiti wa mabanda umiza na kuweka mifumo mizuri ya utoaji taarifa kuhusiana na uhalifu wa kimitandao na urekebishaji wa Sheria ili kuweka misingi mizuri ya Uzuiaji, Ukamataji na Upelelezi wa Makosa yanayohusiana makosa ya ponografia.



***"Hapa Tanzania, kifungu cha 13 na 14 cha Sheria ya Makosa ya Mtandao, 2015 ni kosa la jinai kwa mtu yeyote kujihusisha na ponografia za aina yoyote ile ikiwemo za watoto kwa kuchapisha au kusababisha kuchapishwa au kutoa au kuweza upatikanaji kupitia katika mfumo wa kompyuta picha za ponografia au ponografia za watoto"***

# Matumizi ya Ushahidi wa Kisayansi katika kuthibitisha Makosa ya Unyanyasaji wa Kingono – Changamoto na Malengo.

**Na Valence Shinda Mayenga**
**Wakili wa Serikali Mkuu**

**DHANA YA USHAHIDI WA KISAYANSI KATIKA JINAI.**

Sehemu ya XV ya Kanuni ya Adhabu inatenganisha makosa ya kingono, katika makundi mawili yale kawaida na yale ya kufanya ngono kinyume na maumbile. Umuhimu wa matumizi ya uchunguzi wa kisayansi katika mashauri haya unaonekana katika maamuzi mbalimbali ya Mahakama na kwenye sheria mbalimbali zilizopitishwa na Bunge.

Waendesha Mashtaka na Wapelelezi wanatakiwa kuongeza uelewa kuwa kuna maamuzi na miongozo mbalimbali juu ya namna sahihi ya kuchukua sampuli na kuziwasilisha katika maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya Uchunguzi. Uthabiti huu wa Ushahidi wa kisayansi katika mashauri ya kingono unaweza kutumika katika mazingira mengi na machache kati ya hayo ni ***(1)kusaidia kuongeza nguvu ya kiushahidi pale ambapo hakuna Ushahidi wa moja kwa moja (2) wataalam mbalimbali walioanishwa na sheria kujaza nyaraka za kitaalam zinazosaidia kuthibitisha utendekaji wa kosa, (3) kuwapa wahanga wigo mzuri wa kuwasilisha malalamiko yao mapema ili yachunguzwe kisayansi (4) Matumizi ya Ushahidi wa vinasaba (DNA) (5) kusaidia kubaini changamoto za aina hii ya uchunguzi namna unavyokusanywa, kuchakatwa na kuwasilishwa mahakamani.***

Wachunguzi na waendesha mashtaka wanalo jukumu kubwa sana la kuhakikisha uchunguzi huu wa kisayansi unatumika na kuwasilishwa mahakamani hususani katika mashauri ya unyanyasaji wa kingono.

**UTANGULIZI**

Makosa ya unyanyasaji wa Kingono yanashika kasi katika jamii yetu Pamoja na kuwa adhabu iliyowekwa kwa wanaokutwa na hatia kuwa kali sana. Makosa haya yamekuwa yakifanywa mara nyingi kwa Watoto wa jinsia zote (*wa kike na wa kiume*) Japokuwa haijandikwa popote lakini ukweli ni kuwa kosa linapokuwa na adhabu kali basi linahitaji Ushahidi madhubuti katika kulithibitisha. Katika mazingira haya umuhimu wa matumizi ya Ushahidi wa kisayansi kuwahusisha wakosaji na makosa waliyoyafanya unakuwa wa umuhimu mkubwa.

Kila mmoja wetu ni shahidi juu ya matukio ya unyanyasaji wa kingono yanayoendelea nchini kwetu, mitandao ya kijamii imejaa taarifa za matukio ya unyanyasaji wa kingono unaotendeka kila

siku, wababakaji nao wanafikishwa mahakamani kila siku. Ni aibu kubwa kuwa makosa haya hayabagua yafanyike kwa nani yamuache nani, tumesikia na kuona Watoto wakiwafanyia matendo haya mama zao, wazazi wakiwafanyia Watoto wao wa kuwazaa, walimu wakiwafanyia wanafunzi, watumishi wa dini wakiwafanyia waumini wao, watu wenye mtindio wa ubongo nao hawajaachwa nyuma katika kutendewa masaibu haya, maafisa wa polisi wakiwafanyia mahabusu, madaktari wakiwafanyia wagonjwa n.k pia kuna ongezeko la wimbi la mimba za utotoni kwa wanafunzi wa shule jambo linalopelekea Watoto wengi wa kike kusitisha masomo yao, kutoroka nyumbani na wakati mwingine kupoteza Maisha kutokana na kupata mimba katika umri mdogo mbaya zaidi imekuwa ikiwasababishia kupata maambukizi ya magonjwa ya zinaa kama Ukimwi. Imefika wakati sasa Watoto wamekuwa wakitumika katika biashara ya ngono katika majiji makubwa.

Kutokana na ongezeko hili la ukatili wa kingono, ni wazi kuwa jamii yetu imefikia hatua mbaya ambayo sasa ni jukumu la kila mmoja wetu kulivalia njuga suala hili na kulikemea kwa kadri nafasi yake inavyoruhusu.

Pamoja na ongezeko hili la makosa ya unyanyasaji wa kingono katika nchi yetu, tunazo sheria kali zinazoweka katazo la matendo haya, makatazo mengi yanaonekana katika sehemu ya XV ya **Kanuni ya Adhabu** kuanzia kifungu cha **129A** mpaka kifungu cha **161**. Makosa yanayojirudia mara kwa mara na ambayo tumeyajadili katika makla hii niyale ya Ubakaji, Kulawiti na kuzini na maharimu. Kosa la kumsababishia ujauzito binti wa shule adhabu yake inapatikana katika kifungu cha **60A (3)** cha sheria ya Elimu (The Education Act) kifungu hicho kinasomeka kama ifuatavyo

**60A (3)** *Any person who impregnates a primary school or secondary school girl commits an offence and shall, on conviction, be liable to imprisonment for a term of thirty years.*

Kifungu kilichoainishwa hapo juu kinaonyesha ni kwa namna gani makosa ya unyanyasaji wa kingono yanabeba adhabu kubwa, lengo kuu la makosa haya kubeba adhabu kubwa ni kuwaadhibu vikali wakosaji lakini pia kuwaonya wanaokusudia kufanya makosa haya kuachana na nia hiyo kabisa. Pamoja na uwepo wa adhabu hii kali unyanyasaji wa kingono bado haujakoma, Makala hii haikupata takwimu sahihi juu ya makosa haya lakini kwa kutazama yanayoendelea katika jamii unaweza kusema kuwa makosa haya yanazidi kuongezeka.

Makosa haya wahanga wake wakubwa ni mabinti wa umri mdogo na sababu zifuatazo zinaonyesha ni kwanini wahanga wakuu wa makosa haya ni mabinti wa umri mdogo, **Kwanza** ni *umasikini*, mabinti wengi wananyanyasika kingono wakilipwa ujira mdogo wa fedha ama kupewa vitu vidogo vidogo, wakati mwingine wazazi wamekuwa wakiwaozesha mabinti zao katika umri mdogo ili wapate fedha. **Pili** *kukosa ufahamu*, Watoto wengi wanajihusisha katika vitendo hivi bila kuwa na ufahamu wa yale wanayoyafanya, wengine wanafuata mkumbo na engine wanaona ni starehe tu. **Tatu** *Madhara ya ukuaji wa teknolojia,* matukio mengine yanatokana na kuiga kutokana na yale vijana waliyoyaona katika mitandao ya kijamii ponografia ikiwa ndo kinara katika hili. **Nne** ni matumizi ya dawa za kulevya hili nalo ni tatizo sugu ambalo linapelekea Watoto wengi katika majiji na miji mikubwa kujihusisha kwenye ngono zembe **Tano** *ni Imani potufu*, tumeshuhudia watu wakijihusisha katika vitendo vya ngono katika kutimiza matakwa yao ya kiimani wengine wakiamini kuwa itawaletea bahati na wengine wakiamini watapata mali, hii imekuwa ikihusIsha ubakaji kwa wazazi na Watoto lakini pia watu kuwabaka watu wenye mtindio wa kiakili n.k. **Sita** *Kukimbilia mjini* hii pia ni changamoto kubwa sana inayochangia kukwamisha juhudi za kupambana na makosa haya ya unyanyasaji wa kingono. Kuna ongezeko kubwa la Watoto wanaokimbia toka vijijini Kwenda mijini, mbaya zaidi Watoto hawa hukimbilia mijini wakiwa hawama mwenyeji wala mahala pa kufikia.

Mfano mzuri wa tukio la namna hii ni lile lillotokea Wilayani Tarime, vijana wawili walisafiri kutoka Mwanza kuelekea Tarime kwa njia ya basi, walifika mjini tarime majira ya saa moja na nusu usiku

hawakuwa na mwenyeji wala fedha za kujikimu hivyo waliamua kulala katika korido za vibanda vya maduka vilivyopo katika stendi ya mabasi Tarime. Wakiwa wamelala usiku alifika mtu mmoja na kuwambia awapeleke nyumbani kwake wakalale na wao walikubali, wakiwa njiani wanaenda baada ya kufika sehemu yenye vichaka, mtu huyo aliwageuka na kuanza kuwatendea vitendo vya ngono kinyume na maumbile, Watoto wale walilia wakiomba msaada na mlinzi aliyekuwa karibu na maeneo hayo aliweza kuwaokoa na mtu huyo alitiwa nguvuni. Jambo hili lilitokea katika mji mdogo wa Tarime, unaweza kuona ni kwa kiwango gani janga hili ni kubwa katika miji mikubwa zaidi ambako Watoto wanakimbilia kila siku. **Saba** ni *mmomonyoko wa maadili*, mmomonyoko wa maadili ni jambo jingine ambalo linachangia kwa uhalifu huu kuongezeaka. Wamaume watu wazima kwa sasa hawaoni aibu kuwatongoza mambinti wadogo wenye umri sawa na mabinti zao na kitendo cha Watoto kuwakubalia watu wazima hawa ni ishara nyingine ya mmomonyoko wa maadili katika jamii. Kuna matukio mengine ya unyanyasaji wa kingono yanatokea kutokana na wazazi kutotimiza majukumu yao katika malezi, wakati mwingine unakuta Watoto wanaingia na kutoka nyumbani kwa wazazi wao muda wowote kadri wanavyotaka na kadri wanavyoamua bila kupata pingamizi lolote kutoka kwa wazazi wao.

Makosa haya ya unyanyasaji wa kingoni yanazidi kukithiri katika jamii yetu, bila kuathiri jitihada zingine zinazofanyika kupambana na uhalifu wa aina hii, wahalifu wanapaswa kukamatwa na kushtakiwa na hatimaye kupata adhabu kwa mujibu wa sheria. Kama ilivyo kwa makosa mengine, jukumu la kuthibitisha kuwa mhalifu ametenda kosa liko upande wa mashtaka na kiwango cha uthibitishaji ni kutoacha shaka yoyote yenye maana, ili kukidhi takwa hili la kisheria Ushahidi wa kitabibu ni miongoni mwa ushahidi muhimu sana ili kuthibitisha kama kweli muhanga alitendewa tukio ama kweli mtuhumiwa alihusika kutenda kosa. Sote tunafahamu msimamo wa kisheria unaotumika kwa muda mrefu sasa kuwa Ushahidi mzuri katika makosa ya unyanyasaji wa kingono unatoka kwa mtendewa wa tukio. Hili pia linatiliwa mkazo na kifungu cha 127(6) Sheria ya Ushahidi, sura ya 6 marejeo ya 2022, inapoelezwa kuwa mahakama ikimuamini muhanga wa tukio basi inaweza kumtia hatiani mshtakiwa bila kuhitaji Ushahidi mwingine wa ziada. Hii inaenda mbali zaidi kuonyesha kuwa hata kama Ushahidi wa kitabibu utakuwa haujaleta majibu Chanya dhidi ya malalamiko ya muhanga, bado haiwezi kubatilisha ukweli toka kwa muhanga ambaye ndiye kimsingi alikumbana na kadhia ya unyanyasaji wa kingono, tazama shauri la ***MASALU KAYEYE dhidi ya Jamhuri Rufaa ya Jinai no. 20 ya mwaka 2017 ukurasa wa 21-22***

Japokuwa Ushahidi wa kisayansi au kidaktari kwenye mashauri mengine sio wa lazima, lakini hii haipaswi kuchukuliwa kama ndio utaratibu. Kuna wakati mwingine Ushahidi wa kisayansi haukwepeki ili kuthibitisha hoja katika shauri, kuna mzaingira ambayo unakuta muhanga kwasababu zozote zile kwa mfano umri au mtindio wa ubongo hawezi kutoa Ushahidi mahakamani. Katika mazingira ya namna hii Ushahidi wa kisayansi haukwepeki, mfano mzuri unapatikana katika mashauri yafuatayo, ***MAKENJI KEMURA dhidi ya Jamhuri rufaa ya Jinai nambari 30 ya 2018***, Ushahidi wa Muhanga katika shauri hili ulitupiliwa mbali kwa kuchukuliwa kinyuma na utaratibu lakini Ushahidi wa daktari uliokoa jahazi kuweza kuthibitisha kuwa Muhanga alikuwa ameingiliwa. Pia tazama shauri la ***STEWARD KOSTA @ NGOLE dhidi ya Jamhuri, rufaa ya jinai nambari 42 ya mwaka 2021*** katika shauri hili muhanga alikuwa na umri wa mwaka mmoja na miezi saba tu hivyo hakuweza kutoa Ushahidi wake juu ya madhira yaliyomsibu lakini mtuhumiwa alitiwa hatiani kwa kutegemea Ushahidi wa kitabibu kuthibitisha kuwa alikuwa ameingiliwa.

Makosa ya kumsababishia ujauzito binti wa shule kama yanavyoainishwa kwenye sheria ya Elimu nayo yanatazamwa katika Takakuri mbili tofauti. **Tafakuri ya kwanza** inajikita katika mlengo kuwa kusababisha ujauzito kwa binti wa shule hakuwezi kuthibitishwa kwa maneno matupu, Ushahidi wa kisayansi unatakiwa katika kuthibitisha uhusika wa mshtakiwa na kiumbe kilichopo tumboni. Kwa

mfano katika shauri la ***PETER SILVESTER dhidi ya Jamhuri rufaa ya jinai nambari 205 ya 2019*** mahakama ilisema yafuatayo

"*…What the prosecution was able to prove was that the victim was impregnated. It did not bring concrete evidence to prove that it was the accused, now the appellant, who caused such pregnancy.* ***That would have best been proved by scientific evidence and in the circumstances of the case the DNA test evidence was much appropriate to ascertain the fatherhood of the baby, which evidence in turn would have proved a person liable for impregnating the victim****. In the absence of such kind of evidence it was unsafe to find the appellant guilty of impregnating the victim'. (Emphasis added).*

Msimamo huo wa mahakama umefuatwa pia katika Mashauri yafuatayo

1. ***RWAKI ZACHARIA dhidi ya Jamhuri rufaa ya jinai nambari 23 ya mwaka 2021***
2. ***LUME DANGA dhidi ya Jamhuri rufaa ya Jinai nambari 16 ya mwaka 2022***
3. ***GOROBANI BRANDI @ KATUMBO dhidi ya Jamhuri rufaa ya jinai nambari 86 ya mwaka 2021***

**Tafakuri ya Pili** hii inakinzana na ile tafakuri ya kwanza, tafakuri hii inaamini kuwa kuthibitisha makosa ya kumsababishia ujauzito binti wa shule hapahitajiki Ushahidi wa kisayansi na maamuzi yaliyojitokeza kuunga mkono tafakuri hii ni ***HAMIS MAHENDI dhidi ya Jamhuri rufaa ya jinai nambari 121 ya mwaka 2020*** na shauri la ***MAWAZO KUTAMIKA dhidi ya Jamhuri rufaa ya Jinai nambari 64 ya mwaka 2020***. Mlengo mkuu wa Tafakuri hii wanasema kuwa kama ilivyo kwa makosa mengine ya unyanyasaji wa kingono, kosa la kumsababishia ujauzito binti wa shule linaweza kuthibitishwa kwa kuongea tu. Ukitazama kwa ukaribu tafakuri hizi mbili unaona kuwa kuna mkanganyiko mkubwa juu ya maamuzi ya Mahakama Kuu katika tafakuri hizi mbili. Jitihada zetu kutafuta maamuzi ya mahakama ya Rufaa juu ya matumizi ya Ushahidi wa vinasaba ili kuthibitisha ujauzito hazikuzaa matunda zaidi, ila kuna shauri moja tu la **Mawazo Kutamika** ambalo lilitolewa maamuzi tarehe 24/02/2023.

Kanuni za kisheria zinahitaji maamuzi ya Mahakama za juu kufuatwa na Mahakama za chini (*Doctrine of Precedent*) na kwa mantiki hiyo shauri la **Mawazo Kutamika** lililotolewa maamuzi na mahakama ya rufaa ambalo linasema matumizi ya Ushahidi wa vinasaba sio muhimu katika kuthibitisha makosa ya kumsababishia binti wa shule ujauzito. Lakini hilo sio lengo la Makala hii, Makala hii inalenga kuibua fikra mpya juu ya matumizi ya Ushahidi wa kisayansi katika makosa ya kingono. Tumetazama kwa ukaribu juu ya tafakuri hizi mbili hatuwezi kusema ni tafakuri ipi ni sahihi zaidi, lakini tunaweza kutoa maoni yetu tu. Ni wazi kuwa tafakuri hizi mbili haziwezi kuwa sawa kwa wakati mmoja, lakini kwa mtazamo wetu tunaona kuwa Tafakuri ya kwanza juu ya matumizi ya vinasaba inamashiko. Tunasema hivyo kwasababu kama tulivyotangulia kusema hapo awali, upande wa mashtaka wanalo jukumu la kuthibitisha hoja bila kuacha shaka yoyote yenye maana, katika kufanya hivyo unatakiwa kuwa na Ushahidi wote wa msingi unaoweza kukusaidia kuthibitisha shtaka. Tunaamini kwamba kwa namna yoyote ile kama mshtakiwa ana mahusiano na kiumbe kilichopo tumboni basi ni busara kwa namna ambavyo teknolojia imekua basi kufanya uchunguzi wa kisayansi kuthibitisha hilo, kutokuwepo kwa Ushahidi wa aina hii mahakama inaweza kufanya maamuzi dhidi ya upande wa mashtaka. Changamoto kuu katika matumizi ya aina hii ya Ushahidi ni kuwa itabidi usubiri mtoto azaliwe ili uweze kuchukua vinasaba, hii inatokana na takwa la kisheria linalotokana na sheria Usimamizi wa vinasaba vya binadamu, sheria namba 8 ya mwaka 2009, sheria hii katika kifungu cha 45 inazuia uchukuaji wa sampuli za mama mjamzito isipokuwa pale inapochukuliwa kwa ajili ya matibabu. Sheria hiyo inasema yafuatayo.

45 (1) The Human DNA test shall ***not*** be conducted on a pregnant woman unless the test is for medical purposes.

Kwa maelekezo hayo ya sheria kama vinasaba

vitachukuliwa kwa binti mjamzito kwa ajili ya uchunguzi/upelelezi itakuwa imekiuka matakwa ya sheria na hivyo kufanya Ushahidi huo kutokuwa sahihi kwenye macho ya sheria. Changamoto hii ni kubwa kwani inawalazimu wapelelezi kusubiri miezi tisa mpaka mtoto anapozaliwa, kwa kipindi chote hiki mtuhumiwa atatakiwa kuwa nje kwa dhamana.

## 2. LENGO LA MAKALA HII

Ujumbe unaokusudiwa kupatikana baada ya kusoma Makala hii ni kuwa matumizi ya Ushahidi wa kisayansi katika mashauri ya unyaynyasaji wa kingono ni ya muhimu, na yanaweza kuwa kama daraja kuunganisha mapungufu yaliyopo katika kesi ya upande wa mashtaka. Makala hii itumike kama ukumbusho katika maeneo yaliyojadiliwa lakini pia ifungue macho ya wapelelezi, waendesha mashtaka na waamuzi juu ya ukusanyaji, utunzaji na utumiaji wa Ushahidi wa kisayansi. Makala hii itajadili sheria mbili ambazo ni The Medical, Dental, and Allied Health Professionals Act and The Human DNA Regulation Act. Kupitia sheria hizi uchunguzi wa kisayansi kwenye mashauri ya unyanyasaji wa kingono ndiko unakofanyikia. Umuhimu wa matumizi ya Ushahidi wa kisayansi kwenye mashauri haya ulisemwa katika shauri la ***CRISTOPHER KANDIDIUS @ALBINO dhidi ya Jamhuri, rufaa ya jinai nambari 394 ya mwaka 2015*** mahakama ilisema yafuatayo –

*"Unfortunately, despite the enactment of the Human DNA Regulation Act, 2009 (Act No. 8 of 2009) criminal investigation and prosecution in Tanzania still shy away from comprehensive use of the DNA evidence to fill evidential gaps to solve crimes especially where there is lack of direct evidence"*

Nukuu hiyo hapo juu inajielezea yenyewe hatuhitaji kuweka chumvi nyingi. Katika kurasa zinazofuata tutajadili namna ya ukusanyaji na utumiaji wa Ushahidi wa kisayansi kwa kutumia sheria tajwa hapo juu. **Karibu tusafiri pamoja**.

## 3. SHERIA YA MADAKTARI, MADAKTARI WA MENO NA WATAALAMU WA AFYA SHIRIKISHI (THE MEDICAL, DENTAL, AND ALLIED HEALTH PROFESSIONALS ACT)

Kawaida tukio la uhalifu wa kingono linapowasilishwa katika vituo vya polisi, polisi humpatia fomu namba tatu (PF 3) muhanga kwa ajili ya kumsaidia katika huweka kumbukumbu za matibabu yake. Fomu hii ni maalum na inapatikana katika mwongozo wa utendaji kazi wa Jeshi la Polisi nambari 170 wa mwaka 2021. Mwongozo huu unatolewa na Inspekta Jenerali wa Jeshi la Polisi kwa mamlaka aliyopewa na kifungu cha 7(2) cha Sheria ya Jeshi la Polisi na Huduma saidizi Sura ya 322 marejeo ya mwaka 2002. PF 3 imegawanyika katika sehemu nne, sehemu ya kwanza inajazwa na afisa wa polisi ambaye anaelekeza daktari afanye uchunguzi kwa mgonjwa, daktari anafanya uchunguzi kwa mgonjwa kisha anajaza sehemu ya pili, tatu na nne ya PF 3,

The Medical, Dental, and Allied Health Professionals Act inamtambua mtu anayeweza kujaza PF 3 kwa namna ifuatayo kama inavyoelezewa kwenye vifungu vya 18 na 22

***"A person holding degree, advanced diploma or certificate in medicine or dentistry from an institution recognized by the Council, with his level of competency and registered or enlisted to practice as such…"***

Tafsiri hii ya mtu anayeweza kutoa huduma kwa mgonjwa aliyepewa PF 3 imeainisha kiwango cha elimu anachotakiwa kuwa nacho mtoa huduma. Tafsiri hii ni tofauti na tafsiri iliyokuwa inapatikana kwenye sheria iliyofutwa **Medical Practitioners and Dentists Act (Cap 152 R.E 2002)** sheria hii kwenye kifungu cha pili yenyewe ilitoa tafsiri ifuatayo

**"a *person professing to practice medicine or surgery, or holding himself out as ready and willing to give medical or surgical treatment to patients and that person has to be registered and licensed pursuant to provisions of sections 17 and 22 of the Act"***

Hoja tunayojaribu kujenga hapa ni kuwa wapelelezi wanapaswa kuhakikisha kuwa afisa anayehusika katika ujazaji wa PF 3 anakidhi matakwa ya sheria vinginevyo Ushahidi wake unaweza usipokelewe mahakamani. Makosa ya mara kwa mara yamekuwa yakidhihirika baada ya wauguzi (nurses) kujaza PF 3 wakati sheria haiwatambui, hivyo hawawezi kutoa maoni ya kitaalamu kwenye mashauri ya unyanyasaji wa kingono. Kwa mfano katika shauri la ***HAMIS KAYANDA dhidi ya Jamhuri Criminal Appeal No. 166 la mwaka 2018*** Mahakama ya Rufani ilipoketi Mbeya ilisema muuguzi sio afisa anayeruhusiwa na sheria kujaza PF 3. PF 3 iliondolewa kwenye vielelezo vilivyowasilishwa na upande wa mashtaka, lakini mahakama ilibakiza Ushahidi wa mdomo wa nesi, Ushahidi huo ulibaki sio kama mtaalam bali ulibaki kama mtu ambaye alimshughulikia muhanga wa tukio katika hatua za awali. Matukio mengine ya uhalifu wa ubakaji yanapelekea mpaka kutokea kwa mauaji hivyo kumuhitaji mtaalam kufanya uchunguzi wa mwili wa marehemu na kujaza taarifa ya uchunguzi wa mwili wa marehemu, hali kama hii iliwahi kujadiliwa kwenye shauri la CHARLES BODE dhidi ya Jamhuri rufaa ya jinai nambari 46 ya mwaka 2016 na mahakama ilisema kuwa maafisa Tabibu nao ni miongoni mwa watu wanaoruhusiwa kufanya uchunguzi wa mwili wa marehemu. Japokuwa kifo kinapotokea katika mazingira ya kubaka basi kosa litakalopelekwa mahakamani ni la mauaji japokuwa mauaji yakithibitika kosa la kubaka nalo litakuwa limeadhibiwa moja kwa moja.

### 3.1 Changamoto wanazokabiliana nazo Wapelezi na waendesha Mashtaka katika matumizi ya Ushahidi wa kisayansi.

Kuna changamoto mbalimbali wanakumbana nazo wapelelezi na baadaye waendesha mashtaka katika upatikanaji na matumizi ya Ushahidi wa kisayansi kwa wahanga wa unyanyasaji wa kingono.

i. **Kuchelewa kutoa taarifa ya tukio,** kuna nyakati wahanga huwa wanafika kituo cha polisi kutoa taarifa ya tukio wakiwa wamechelewa sana mfano siku kadhaa baada ya tukio kutokea, hii huathiri namna nzuri ya kupata Ushahidi wa kisayansi unaotakiwa kwa kuwa baadhi ya dalili zinakuwa zimeshapotea au kufutika kabisa, wakati mwingine ucheleweshaji huu wa taarifa umekuwa ukiathiri kesi ya upande wa mashtaka hasa pale kunapokosekana sababu za msingi za kwanini muhanga alikawia kuwasilisha taarifa kituo cha polisi.

ii. **Uchunguzi wa kitabibu kwa muhanga kuchelewa.** Kumpatia PF 3 muhanga ni suala moja na muhanga Kwenda hospitali ni suala lingine, wakati mwingine wahanga wanapewa PF 3 waende hospitali lakini hawaendi kwa wakati unaotakiwa, hii huchangia kwa mgonjwa kupata maambukizi zaidi na mimba zisizotarajiwa. Sababu kubwa inayochangia ni umasikini, uchunguzi unaohusisha jeshi la polisi nao unahitaji kulipiwa, hivyo pale ambapo familia ya muhanga inakuwa haijajiandaa ipasavyo katika kuhudumia matibabu ya muhanga inaweza ikachukua muda familia kutafuta pesa ili kumpatia matibabu muhanga.

iii. **Ujazaji usiokidhi matakwa wa PF 3.** Baadhi ya wahudumu wa afya wanakosa ufahamu na uzoefu juu ya namna ya kujaza PF 3, wakati mwingine sehemu yanayotakiwa kujazwa kwenye sehemu ya tatu yanajazwa kwenye sehemu ya nne ya PF 3. Hii inapelekea upelelezi kuchukua muda mrefu kwani jalada linapofikishwa Ofisi ya Mashtaka kwa ajili ya maamuzi, mwendesha mashtaka analazimika kulirudisha kwa ajili ya marekebisho kwenye PF 3, muda mwingine mapungufu hayo hayabainiki mapema na kukuta tayari PF 3 imeshatolewa mahakamani kama kielelezo.

iv. **Kutofuata taratibu za kutoa kielelezo**

**mahakamani.** Utoaji wa vielelezo vya kinyaraka Mahakamani kama PF 3 una taratibu zake, na siku za hivi karibuni kumekuwa na ukiukwaji wa taratibu hizo, utoaji wa vielelezo vya kinyaraka unapitia hatua tatu muhimu ambazo ni, **moja** *kuitambua na kuielezea nyaraka kabla haijapokelewa,* **mbili** *ni kupokelewa mahakamani* na **tatu** *kuisoma nyaraka hiyo mahakamani baada ya kupokelewa kama kielelezo.* Utaratibu huu umekuwa ukikiukwa katika mashauri mengi hivyo kupelekea PF 3 kuondolewa kama sehemu ya kielelezo pale inapofika hatua ya rufaa.

v. **Kutozingatia matakwa ya kifungu cha 240 cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai.** Kifungu cha 240 cha sheria tajwa hapo juu kinaruhusu taarifa za kitabibu kutolewa na mtu mwingine hata kama sio mtaalamu wa tiba ambaye alihusika na kuandaa nyaraka hiyo. Lakini kifungu cha 240(3) cha Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai kina taka Mahakama kumtaarifu mshtakiwa haki yake ya kuamua kama anamuhitaji afisa aliyehusika na ujazaji wa taarifa hiyo ya kitabibu kwa ajili ya maswali ya dodoso. Kwenye baadhi ya mashauri takwa hili la kisheria halizingatiwi na hivyo kupelekea kielelezo husika kuwekwa kando wakati wa rufaa.

## 4. SHERIA YA UDHIBITI WA VINASABA VYA BINADAMU, 2009 (THE HUMAN DNA REGULATION ACT, 2009).

Sheria hii inatoa miongozo ya namna ya kukusanya, kufungasha, kusafirisha, kuhifadhi, kuchambua na kuharibu sampuli za vinasaba vya binadamu. Vinasaba vya binadamu maana yake ni asidi ya Deoksiribonucleic ambayo ni nyenzo ya kijenetiki iliyopo kwenye kiini cha seli na mitochondria ambayo hurithiwa nusu kutoka kwa kila mzazi kibaolojia (***tafsiri hii ni kwa mujibu wa kifungu cha tatu cha sheria ya udhibiti wa Vinasaba vya Binadamu, 2009****)*. Ushahidi wa vinasaba vya binadamu katika uthibitisho wa mashtaka ya jinai ulitumika kwa mara ya kwanza katika kesi ya mauaji ya ***JOSEPH LUGATA dhidi ya Jamhuri rufaa ya jinai namba 317 ya mwaka 2009.*** Katika Shauri hili, Mrufani wakati wa upelelezi, alikutwa na fulana na kofia iliyokuwa na damu. Wasifu wa sampuli za damu kutoka kwa watoto wa marehemu na mali zilizokamatwa zililingana baada ya uchambuzi hivyo kuhusisha mshtakiwa/mrufani na kifo cha marehemu. Kuhusiana na matumizi ya ushahidi wa vinasaba vya Binadamu Mahakama ilisema kwamba ni muhimu kila mara kuwa na ushahidi mwingine huru ambao unaweza kumtia hatiani mshtakiwa mbali na kipimo cha vinasaba.

Katika uchunguzi wa makosa ya jinai, vinasaba vya binadamu vinaweza kukusanywa na kuchunguzwa kwa ajili ya kuthibitisha utambulisho wa mtu (**HID** yaani Human Identification), wazazi ama mambo mengine yanayoweza kukutwa eneo la tukio. Katika uchunguzi wa aina hii sampuli za aina mbili zinaweza kutumika, sampuli ya aina ya kwanza ni zile sampuli za ndani (*intimate sample*) ambazo zaweza kuwa damu, manii au majimaji mengine ya tishu, ama nywele zingine zinazopatikana sehemu iliyofichika ya mwili wa mwanadamu. Sampuli aina ya pili ni ile ambayo sio ya ndani (*non – intimate*) sampuli za aina hii zinaweza kuwa ni mate, mkojo, nywele za nje ya mwili, kucha au vitu kutoka chini ya kucha, nyayo za mguu au mkono n.k. jambo muhimu la kuzingatia hapa ni kuwa sampuli hizi za vinasaba lazima zichukuliwe na afisa anayetambulika na sheria. Kwa ajili ya upelelezi afisa anayetambuliwa na sheria kuchukua sampuli ni Mkuu wa Kituo (OCS) ama afisa mwenye cheo cha juu zaidi ya Mkuu wa Kituo ama afisa wa polisi aliyeidhinishwa na Waziri wa Mambo ya Ndani kwa ajili ya kukusanya sampuli za vinasaba. Kwa msingi huo ni kosa kisheria kwa sampuli za vinasaba vya binadamu kukusanywa na mtu

ambaye hatambuliki kisheria.

Sampuli hizo baada ya kukusanywa zinapelekwa kwenye maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali ama maabara maalumu iliyoidhinishwa kwa ajili ya uchunguzi wa vinasaba vya Binadamu. Maombi ya uchunguzi wa vinasaba lazima yafanyike kwa maandishi na kwa upelelezi unaofanywa na Jeshi la Polisi afisa mwenye mamlaka ya kufanya maombi ni Afisa wa Polisi mwenye cheo cha Inspekta wa Polisi na kuendelea. Kama maombi yatafanywa na Afisa ambaye hajatajwa na sheria basi maombi hayo ni batili na hayawezi kutumika kuthibitisha hoja Mahakamani. Kama ilivyo kwa Ushahidi mwingine, ukusanyaji, ufungashaji, usafirishaji na upembuzi wa vinasaba lazima uainishwe wakati wa usikilizaji wa shauri husika ili kuweza kuonyesha kuwa kielelezo kilichofikishwa mahakamani ndicho hasa kilipatikana kutokana na tukio linalobishaniwa. Kushindwa kuonyesha mtiririko huu kwa ufasaha kunaathiri thamani ya kielelezo hicho pale mahakama inapokuwa inakitegemea kufanya maamuzi.

## 5. HITIMISHO

Katika Makala hii kwa ufupi tumeangazia uhusiano uliopo juu ya uchunguzi wa kisayansi na uthibitishaji wa mashauri ya jinai, tumeainisha ni kwa namna gani Ushahidi unaweza kukusanywa na kuwasilishwa Mahakamani. Hii ni katika uwanda mzima wa matumizi ya teknolojia kuendana na kasi ya ulimwengu ambapo teknolojia inaweza kutumika kuwatia hatiani wakosaji na kuwaondoa hatiani wale wasiokuwa na hatia. Makala hii haikuwa inakusudia kulinganisha mambo haya mawili bali ililenga kuonyesha umuhimu wa matumizi ya Ushahidi wa kisayansi katika kuthibitsha mashauri ya jinai. Jambo la kufurahisha ni kuwa Pamoja na kuwa Sheria ya Udhibiti wa Vinasaba vya Binadamu , 2009 (The Human DNA Regulation Act, 2009). Imeanza kutumika kwa takribani miaka 15 sasa lakini matumizi yake katika kesi za unyanyasaji wa kingono ni madogo mno.

Kwa kuzingatia mapungufu tuliyoyabainisha hapo juu, tunayo mapendekezo mawili ili kuweza kutibu mapungufu hayo

1. Matumizi ya Uchunguzi wa Vinasaba vya binadamu, tunapendekeza ongezeko la matumizi ya uchunguzi wa vinasaba kwani kama ukifanyika kwa ufasaha utasaidia kuondoa changamoto nyingi zilizopo katika jamii yetu lakini pia itasaidia kuwatia hatiani wenye hatia na kuwaondoa hatiani wasiokuwa na hatia. Pia kutokana na namna uhalifu wa kingono unavyofanyika na upelelezi wake kuwa wa kiwango cha chini, ni wakati muafaka sasa kutumia Ushahidi wa vinasaba katika kuthibitisha makosa ya aina hii.

2. Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kama taasisi yenye mamlaka ya kuratibu uchunguzi na upelelezi wa makosa ya jinai, inapaswa ijikite katika kuwaogoza wapelelezi wa makosa ya kingono kutumia uchunguzi wa vinasaba miongoni mwa uchunguzi mwingine wanaokuwa wanaufanya. Hatua hii itasaidia kuziba pengo lililopo kati ya uchunguzi unaofanyika na mashtaka yanayowasilishwa mahakamani, pia kubadilisha simulizi iliyopo kuwa ushahidi wa muhanga unatosha kumtia hatiani mshtakiwa bila kujali kuwa Ushahidi huo unaweza kuwa na changamoto. Changamoto ya mashahidi wasioweza kutoa ushahidi japokuwa ni waathirika wa ukatili wa kingono pia inaweza kutatuliwa kwa matumizi ya ushahidi wa aina hii, kwa mfano wahanga viziwi, wenye mtindio wa ubongo Watoto wadogo na mabubu. Pia Mafunzo ya mara kwa mara kwa wapelelezi na waendesha mashtaka kuhusu ushahidi wa kisayansi utaleta tija kwani baadhi ya kesi hupata changamoto kutokana na weledi mdogo katika eneo hili.

# HABARI PICHA



*Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana Kileo akimkabidhi zawadi ya tuzo Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Bw. Sylvester Mwakitalu ambayo imetolewa na Chama cha Wafanyakazi (TUGHE) Tawi la Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwa niaba ya Watumishi wote wa Ofisi hiyo ikiwa ni ishara ya kuthamini mchango wake katika kuleta mabadiliko ya Taasisi, kujali maslahi ya watumishi na kuboresha mazingira ya kazi.*



*Wanawake kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakikabidhi vifaa mbalimbali kwa Muuguzi Mfawidhi kutoka Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Dodoma Bw. Stanley Mahundo vitakavyowasaidia wagonjwa wenye uhitaji waliopo katika hospitali hiyo ikiwa ni ishara mojawapo ya kufanya matendo ya huruma.*



*Mkurugenzi wa Mashtaka Bw. Sylvester Mwakitalu, Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Bw. Ramadhani Kingai, Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU Bw. Crispin Chalamila, Kamishna Generali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Bw. Aretas Lyimo, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bi. Bibiana Kileo wakifuatilia taarifa ya hali ya Magereza kutoka kwa Mkuu wa gereza la Mahabusu la Keko, Kamishna Msaidizi Juma Mgumba wakati walipotembelea gereza la Mahabusu Keko Jijini Dar es salaam tarehe 19 Novemba, 2024.*



*Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Bw. Sylvester Mwakitalu (katikati) na Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Bi. Bibiana Kileo (watatu kushoto) wakiwa na washiriki wa mafunzo ya Upelelezi wa makosa ya Uhalifu wa Kifedha yaliyofanyika tarehe 2 Septemba, 2024 Jijini Dar es Salaam.*

*Watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Arusha na baadhi ya wawakilishi wa TUGHE kutoka baadhi ya Mikoa wameungana na Wafanyakazi wengine kuadhimisha Siku ya Wafanyakazi Duniani iliyofanyika tarehe 1 Mei, 2024 katika viwanja vya Sheikh Amri Abeid Jijini Arusha.*





*Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bara Bi. Bibiana Kileo (kulia) akizungumza na Watumishi wa Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Bara na Mahakama ya Tanzania (hawapo pichani) wakati wa ziara ya kutembelea Makao Makuu ya Mahakama Jijini Dodoma iliyofanyika tarehe 14 Agosti, 2024. Kulia kwake ni Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Zanzibar, Bi. Mwanamkaa Mohammed.*

# Miaka Arobaini na Nne (44) ya Kesi ya Waziri Amani

**Na Ignas Mwinuka, Ofmedy Mtenga**

**Mawakili wa Serikali**

## UTANGULIZI

Tarehe 6 Mei 1980, Mahakama ya Rufani iliyoketi Arusha ilitoa maamuzi yaliyobariki kutiwa hatiani na hukumu ya Kifo aliyopewa Mrufani Waziri Amani katika Mahakama Kuu Kanda ya Arusha ambapo awali Mrufani alishtakiwa kwa kosa la Mauaji ya Kukusudia katika Mahakama Kuu Kanda ya Arusha. Waziri Amani alishitakiwa kwa Mauaji ya kukusudia ya DAUD S/O MEKASI lililotokea tarehe 25 Desemba 1975 katika Kijiji cha Mwangalile – Kahe Wilaya ya Moshi Mkoani Kilimanjaro. Baada ya kutoridhishwa na kutiwa hatiani Waziri Amani aliwasilisha Rufaa katika Mahakama ya Rufaa akipinga kutiwa hatiani na adhabu iliyotolewa.

## HOJA/MALALAMIKO KATIKA RUFAA

Waziri Amani kupitia uwakilishi wa Wakili Msomi Mr. Kapoor aliwasilisha hoja mbili za Rufaa, hoja ya kwanza alidai kuwa alitiwa hatiani kwa kuegemea ushahidi dhaifu wa utambuzi. Kwa maelezo kuwa tukio lilitokea usiku na ushahidi uliotolewa haukuweza kukidhi vigezo vya utambuzi.

Hoja ya pili ilikuwa, kulikuwa na kukinzana kwa ushahidi kwa maelezo kuwa kulikuwa na kuhitilafiana kwa ushahidi kuhusiana na maeneo yapi katika mwili wa marehemu kulikuwa na kovu kwani mashahidi watatu wa upande Mashtaka walieleza kuwa marehemu alidhuriwa upande wa kushoto wa kifua ilihali ushahidi wa Daktari ulionyesha Marehemu alidhuriwa Mgongoni.

## UAMUZI WA MAHAKAMA YA RUFAA

Katika uamuzi wake kuhusiana na hoja ya utambuzi iliyowasilishwa, Mahakama ya Rufaa ilitoa vigezo vifutavyo vya kuzingatiwa wakati wa kutathmini uhakika wa ushahidi wa utambuzi ikiwamo; ni muda gani mashahidi walishuhudia tukio, kama ni usiku au mchana? Je ni umbali gani shahidi aliyeshuhudia alikuwepo? kwa chanzo kipi cha Mwanga? na Je mshtakiwa aliwahi kufahamika kwa mashahidi kabla ya tukio au la?

Mahakama iliona kuwa kwa kuangalia ushahidi uliotolewa Mahakamani na upande wa mashtaka na kwa kuangalia maswali ya dodoso yaliyoulizwa na kujibiwa na Waziri Amani, alitambuliwa vyema wakati wa tukio. Na kuhusiana na hoja ya pili ya kukinzana kwa ushahidi kuhusiana na maeneo ambayo marehemu alidhuriliwa, Mahakama iliona maeneo ambayo mashahidi watatu upande wa Mashtaka waliyazungumzia yalikuwa ni maeneo sahihi tofauti na yale yaliyozungumziwa na Daktari katika Taarifa ya uchunguzi wa kifo hivyo waliona hoja hii ilikosa mashiko.

## ASILI YA KANUNI ZA UTAMBUZI

Mahakama ya Rufani wakati ikitoa vigezo vya utambuzi haikurejea shauri lolote lililowahi kuamriwa hapo kabla hivyo ni rahisi kusema kwamba kanuni hizi za utambuzi katika tasnia ya jinai nchini zilitolewa kwa mara ya kwanza katika shauri la Waziri Amani.

Hata hivyo kanuni hizo za utambuzi zilizotajwa ikiwamo za kuthibitisha muda gani mashahidi walishuhudia tukio? Je ni kwa umbali gani? kwa chanzo kipi cha Mwanga? na Je mshtakiwa aliwahi kufahamika kwa mashahidi kabla? katika uthibitishaji wa utambuzi zinaoonekana zilishawahi kutolewa au kuamriwa hapo kabla katika shauri la

***R v Turnbull [1977] QB 224*** katika Mahakama ya Rufaa huko Uingereza, shauri ambalo mpaka sasa linatumika kama shauri la msingi katika rejea katika uthibitishaji wa utambuzi kama ilivyo kwetu katika shauri la ***Waziri Amani v. Republic [1980] TLR 250***

**HITIMISHO.**

Tangu Mwaka 1980 ambapo uamuzi huu utolewe na Mahakama ya Rufaa, mpaka sasa shauri hilo limebaki kama shauri la msingi katika rejea katika kuthibitisha utambuzi wa washtakiwa. Na kimsingi shauri hili limechukua umarufu mkubwa kwani limekuwa likitumika sana miongoni mwa Waendesha Mashtaka, Mawakili wa kujitegemea na watoa maamuzi kwa maana ya Waheshimiwa Majaji na Mahakimu kwa rejea mahakamani na hivyo ni aghalabu sana kwa mwanasheria anayejishughulisha na kesi za jinai kutofahamu misingi ya kinanuni ya shauri la Waziri Amani.

# Mathias Bundala na Sakata la Kumuua Mke Wake Mdogo Kwa Wivu wa Mapenzi

**Na Tawabu Yahya Issa**
**Wakili wa Serikali**

Ilikuwa ni tarehe 26/10/1995 siku nne tu kabla ya uchaguzi Mkuu wa kwanza wa vyama vingi. MATHIAS BUNDALA alimuua Mkewe wa Pili Bi Sarah Stephen. Mauaji haya yalifanyika katika kijiji cha Mwisole kata ya Lutenda wilaya na mkoa wa Tabora. Mathias alikuwa ni Afisa Tabibu na alikuwa akiendesha biashara ya Zahanati inayoitwa Wazazi Zahanati wakati Bi Sarah alikuwa ameajiliwa kama Muuguzi katika Zahanati hiyo. Kwasababu alizozifahamu vizuri Bwana Mathias mwenyewe alimuua mkewe na kumtupa kwenye Shimo la kukatia mbao kisha kuufukia mwili wake. Fununu zilianza kusambaa kuwa Bwana Mathias amemuua mkewe huyo mdogo (Sarah), katika hali ya kushangaza Kaka wa Bwana Mathias , ndg. Robert Bundala alimtaarifu Mwenyekiti wa eneo hilo Bw. Pastory Ngasa kuwa kuna uwezekano mdogo wake kamuua Mkewe. Tarehe 29/10/1995 majira ya jioni baada ya uvumi kuzagaa sana juu ya kutoonekana kwa Sarah , Mwenyekiti aliamua kuwataarifu Polisi, ASP Francis Masawe akiwa katika kituo cha kupigia kura kwa uchaguzi uliokuwa unafanyika kesho yake aliondoka eneo hilo ili kushughulikia taarifa za kifo cha Sarah. Na katika kufanya haya walianzia nyumbani kwa Bwana Mathias Bundala kumuhoji juu ya pahala alipo mke wake. Mathias baada ya kuulizwa hakuwa na majibu yanayoeleweka na alionyesha wasiwasi mkubwa. Jambo hili lilimfanya ASP Francis kuwa mkali kidogo na mwishowe Bwana Mathias aliwapeleka pahala alikokuwa amefukia mwili huo. Giza lilikuwa limeingia lakini walifukua na walipoona mwili waliamua kumtia Mathias nguvuni na kesho yake walifika na Daktari eneo hilo kwa ajili ya kufukua Mwili. Dr Ruben Nyanga baada ya mwili kufukuliwa alishindwa kuufanyia mwili uchunguzi kuweza kubaini sababu ya kifo kwakuwa ulikuwa umeanza kuoza lakini ulitambulika kuwa ni mwili wa Sarah Stephen. Huo ndio ulikuwa mwanzo wa bwana Mathias Bundala kushtakiwa na ushahidi wa upande wa mashtaka ulikuwa ni wa kimazingira (circumstancial) kuwa aliyemuua Sarah ni Mathias, baada ya usikilizaji wa kesi, Mathias alikutwa na kesi ya kujibu na katika

utetezi wake alileta utetezi kuwa yeye hakuwepo eneo la tukio wakati Mkewe anakutwa na umauti (*defence of alibi*) Waungwana wazee wa Baraza walisema Bundala hakuwa na hatia kwakuwa hakuna aliyemuona akitekeleza mauaji hayo na pia kuwa sababu za kifo cha marehemu hazikuainishwa. Jaji Mwita alikuwa na maoni tofauti na waungwana wazee wa baraza na alimtia hatiani Mathias na kusema ushahidi ulikuwa wa kimazingira, pia taarifa za kujikanganya kwa bwana Bundala juu ya mahala alipo Sarah.. lakini pia kuwa Bwana Bundala utetezi wake wa kutokuwepo eneo la tukio haukutia doa ushahidi wa upande wa Mashtaka. Mathias Bundala akawa amehukumiwa na Mahakama Kuu Kanda ya Tabora kunyongwa mpaka kufa. Bwana Bundala hakuridhishwa na Hukumu hiyo hivyo akakata rufaa Mahakama ya Rufani Tanzania na ikawa imezalishwa Kesi Maarufu sana katika uwanda wa Haki Jinai MATHIAS BUNDALA VS THE REPUBLIC, CRIMINAL APPEAL NO. 62 of 2004 CAT at MWANZA

Tarehe 26/02/2007 saa mbili asubuhi gari kutoka gereza la Butimba likiwa limebeba wafungwa na Mahabusu akiwemo Mathias Bundala lilifika Mahakama Kuu Mwanza maeneo ya Kamanga. Mathias Bundala kesi yake Rufaa iliitwa na Naibu Msajili wakati huo S.M Rumanyika na kupitia Wakili Msomi Galati, Bwana Bundala aliwasilisha sababu zifuatazo ili kuonekana hana hatia

i) sababu ya kifo cha marehemu haikuainishwa

ii) hakukuwa na shahidi wa kuona kwa macho aliyeshuhudia Bundala akimuua Sarah

iii) ushahidi wa mashahidi wa mashtaka ulikuwa unajichanganya sana Jamhuri katika rufaa hii iliwakilishwa na Bw. Mdemu (Wakili wa Serikali). Jambo la kufurahisha ni kuwa S.M Rumanyika ambaye alikuwa Naibu Msajili na Mr Mdemu (wakili wa Serikali) kwa sasa wote ni Majaji wa Mahakama ya Rufani. Tuendelee Mr Mdemu alisema rufaa ya bwana Bundala haina mashiko na sababu zake hazina mashiko pia hivyo itupiliwe mbali na hatia na adhabu yake ya kunyongwa mpaka kufa iendelee. Majaji wa Rufani walikubaliana na hoja za Wakili Mdemu (wakati huo) na walisema kuwa;- **Kwanza** sio takwa la kisheria kuwa sababu ya kifo lazima iainishwe katika kila mauaji, Mahakama ya Rufani wanaamini kuwa kifo kinaweza kuthibitishwa kwa ushahidi wa kimazingira bila kuleta mwili wa marehemu au taarifa ya uchunguzi wa mwili wa Marehemu. **Pili**, kuhusiana na kutokuwa na shahidi wa kushuhudia mauaji yakitendeka Mahakama ya Rufani ilisema kuwa kama kila mauaji yanapaswa kushuhudiwa kwa macho basi wauaji wengi wataondoka bila kuadhibiwa kwakuwa wanaamini kuwa mauaji yanaweza kuwa ya namna nyingi, mtu anaweza kuuawa kwa sumu, kuzama majini, njaa n.k hivyo mauaji sio lazima yashuhudiwe kwa macho. **Tatu**, kuhusu mkanganyiko wa mashahidi katika kutoa ushahidi wao, Mahakama ya rufani inaeleza kuwa inaruhusiwa kwa mtu kuwa amesahau baadhi ya vitu kibinadamu pale anapokuwa anatoa ushahidi baada ya muda mrefu tukio kutokea (*katika shauri hili mashahidi walitoa ushahidi miaka tisa baada ya tukio kutokea*) hivyo dosari ndogondogo zinaweza kutokea katika maelezo ya mashahidi na zinaruhusiwa. Mahakama ya rufani inamalizia kwa kusema kuwa ushahidi wa kimazingira hauchukuliwi kama mnyororo wa baiskeli kwamba kiungio kimoja kikikatika basi mnyororo hauwezi kufanya kazi, bali, wanasema kuwa ushahidi wa kimazingira unapaswa kutazamwa kama nyuzi za kamba kwamba uzi ukiwa mmoja unaweza usihimili mzigo lakini zile nyuzi zikiunganishwa kwa pamoja zinaweza kuhimili mzigo mkubwa zaidi na kuwa ya manufaa. Hivyo walivyopitia ushahidi wa kimazingira uliowasilishwa na Jamhuri katika shauri la Mathias wanaona ushahidi huo ukisomwa kwa pamoja haupati tafsiri nyingine, ila, kuwa Bwana Mathias Bundala alimuua kwa kukusudia mkewe mdogo Bi. Sarah Stephen. Mahakama ya Rufani iliendeleza hatia ya Bwana Bundala na Adhabu yake ya kunyongwa mpaka kufa iliendelezwa. Mahakama ya Rufani ni mahakama ya mwisho.

# Uendeshaji wa Mashauri ya Wanyama Pori: Uombaji na Utolewaji wa Amri za Uteketezaji wa Nyara Zinazoharibika Kwa Haraka

**Na Clarence J. Mhoja**
**Wakili wa Serikali**

**1. UTANGULIZI**

Kama ilivyo katika mashauri ya kawaida ya jinai, katika mashauri yahusuyo wanyamapori, hususani yale ya kukutwa na nyara za serikali, vielelezo vya aina mbalimbali hutolewa na upande wa Jamhuri kwa lengo la kuthibitisha kosa. Baadhi ya nyara na vielelezo vinavyokuwa vimekamatwa na watuhumiwa mfano nyama, wanyama au sehemu za wanyama waliouawa haviwezi kuhifadhiwa kusubiri kutolewa kama vielelezo Mahakamani wakati wa usikilizwaji wa shauri kutokana na hali ya kuharibika kwa haraka. Katika mazingira haya, sheria imeruhusu vielelezo hivi vinavyoharibika haraka kuteketezwa kwa amri ya Mahakama. Amri ya uteketezaji wa kielelezo ndio hutumika wakati wa usikilizwaji wa shauri husika badala ya kielelezo ambacho mtuhumiwa anadaiwa kukutwa nacho. Mahakama ya Rufaa katika shauri la Rufaa ya Jinai Namba 168 ya 2019 baina ya ***Ngasa Tambu dhidi ya Jamhuri*** ilisisitiza kuwa ushahidi pekee utakaoweza kuthibitisha kuwa kulikuwa na kielelezo kabla ya uteketezwaji wake ni nyaraka itambulikayo kama inventori ambayo hubeba amri inayoruhusu uteketezaji wa kielelezo hicho. Kwa mantiki hiyo, pale inapotokea, kielelezo husika hakipo na hakuna inventori na amri ya uteketezaji au kuna dosari ya kisheria kuhusu amri ya uteketezaji, basi shtaka la kupatikana na nyara za serikali haliwezi kuthibitishwa.

**2. UOMBAJI WA AMRI ZA KUTEKETEZA NYARA NA VIELELEZO VINAVYOHARIBIKA HARAKA**

Maombi ya kuteketeza nyara na vielelezo vinavyoharibika haraka yanaweza kuwasilishwa kipindi ambapo upelelezi unaendelea au wakati wowote mara baada ya shauri kufunguliwa Mahakamani. Maombi yanaweza kufanywa kupitia kifungu cha 101(1) cha Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori [Sura ya 283 Marejeo ya 2022] ambacho kinaipatia mahakama mamlaka ya kutoa amri ya kuteketeza vielelezo vinavyoharibika haraka wakati wa upelelezi kabla ya mashtaka kufunguliwa mahakamani au baada ya mashtaka kufunguliwa mahakamani. Mwongozo wa namna ya kufanya maombi ya kuteketeza vielelezo kabla kesi haijafunguliwa mahakamani umetolewa pia

katika Aya ya 25 ya Kanuni ya 229 ya Mwongozo wa Utendaji Kazi wa Jeshi la Polisi Tangazo la Serikali Na. 315 la 2021 (PGO).

- Utaratibu wa Kuteketeza Kielelezo Kabla Kesi Haijafunguliwa Mahakamani

Kifungu cha 101(1) (a) cha Sheria ya Hifadhi ya Wanyamapori [Sura ya 283 Marejeo ya 2022] ambacho kinaipatia Mahakama mamlaka kutoa amri ya kutekeketeza vielelezo vinavyoharibika haraka hakijaweka utaratibu wa kufuatwa wakati wa kufanya maombi ya kuteketeza vielelezo kabla kesi haijafunguliwa mahakamani. Utaratibu ambao unaongoza katika kufanya maombi haya na ambao unakubalika na mahakama ni ule ambao umebainishwa katika aya ya 25 ya Kanuni ya 229 ya Mwongozo wa Utendaji Kazi wa Jeshi la Polisi Tangazo la Serikali Na. 315 la 2021 (PGO). Ili mahakama iweze kutoa amri ya kutekeketeza kielelezo, Kanuni ya 229 inaweka utaratibu kwamba kielelezo kiwasilishwe mahakamani pamoja na mtuhumiwa kwa ajili ya mahakama kukiona na kutoa amri ya kuteketeza.

Maombi ya kuteketeza kielelezo kinachoharibika, kama ilivyo kwa maombi mengine ya kimahakama, hufanyika kwa njia ya mdomo au maandishi. Iwapo maombi haya yatafanyika kwa njia ya mdomo, mtuhumiwa atapelekwa mbele ya Hakimu pamoja na kielelezo husika na fomu ya inventori. Baada ya mtuhumiwa kufikishwa Mahakamani, mpelelezi au mwendesha mashtaka atafanya maombi kwa njia ya mdomo ambapo ataeleza kwa ufupi madhumuni ya kufanya maombi hayo, mazingira ya upatikanaji wa kielelezo na hali ya kielelezo kwamba hakiwezi kutunzwa kusubiri usikilizwaji wa kesi ya msingi. Baada ya maelezo hayo Hakimu atakiangalia kielelezo kinachoombewa amri ya kuteketezwa pamoja na inventori na kisha kumuuliza mtuhumiwa iwapo ana jambo lolote la kusema juu ya kielelezo husika na maombi yaliyowasilishwa. Hakimu atapaswa kurekodi yale yatakayoelezwa na mtuhumiwa nyuma ya fomu ya inventori iliyowasilishwa mahakamani. Hakimu atamtaka mtuhumiwa aweke saini yake au alama ya dole gumba kwenye fomu ya inventori. Iwapo mtuhumiwa hatokuwa tayari kuweka saini yake, basi Mahakama itaandika nyuma ya fomu kuwa mtuhumiwa amekataa kuweka saini na sababu, kama itakuwepo. Kisha Hakimu atatoa amri ya kuruhusu uteketezaji wa kielelezo na atasaini na kugonga muhuri wa Mahakama.

Utaratibu wa kufanya maombi ya kuteketeza vielelezo kabla kesi haijafunguliwa mahakamani umefafanuliwa vizuri katika kesi ya ***Buluka Leken Ole Ndidai na Mwenzake dhidi ya Jamhuri, Rufaa ya Jinai Na. 459 la 2020*** Mahakama ya Rufani Arusha (*ukurasa wa 15 hadi 16*) ambapo pamoja na mambo mengine mahakama imesisistiza kwamba wakati wa kutoa amri ya kuteketeza kielelezo mtuhumiwa awepo na ashirikishwe kwa kupewa nafasi ya kutoa maoni au pingamizi kuhusu maombi ya kuteketeza kielelezo husika na majibu yake yaandikwe kwenye inventori au karatasi nyingine na kisha isainiwe na hakimu.

Maombi ya utekeketezaji wa kielelezo pia yanaweza kufanyika kwa njia ya maandishi kupitia kifungu cha 101(1)(a) cha sheria ambapo, mpelelezi au mwendesha mashtaka ataanda maombi kupitia hati ya maombi (chamber summons) ikiwa imeambatana na kiapo na kuwasilishwa Mahakamani. Wakati hati ya maombi itaonesha dhamira ya kuomba uteketezaji wa nyara, kiapo kitaelezea mazingira ya upatikanaji wa nyara, wahusika waliokutwa na nyara husika, mazingira ya kutowezekana kutunza nyara husika kusubiri usikilizwaji wa kesi ya msingi. Mara baada ya maombi kufunguliwa, siku ya kusikilizwa kwake, itawapasa maafisa wakamataji kufika mahakamani wakiwa na mtuhumiwa pamoja na kielelezo kinachoombewa amri ya kuteketezwa. Mahakama itasikiliza maombi na kumshirikisha mtuhumiwa kama inavyofanya wakati wa kusikiliza maombi ambayo yamewasilisha kwa njia ya mdomo. Baada ya kusikiliza maombi, Mahakama itatoa amri ya kuteketeza kielelezo ambayo itatekelezwa na Mkurugenzi wa Wanyama Pori au maafisa waliodhinishwa na Mkurugenzi wa Wanyamapori – soma Rufaa ya Jinai Na. 119 ya 2022, baina ya ***Idd Hamis dhidi ya Jamhuri***, Mahakama ya Rufaa iliyoketi Dodoma katika kurasa wa 9 pamoja

na vifungu vya na 3, 7(1),(4) na 101(1)(a) vya Sheria ya ya Hifadhi ya Wanyamapori [Sura ya 283 Marejeo ya 2022].

- Utaratibu wa Kuteketeza Kielelezo Baada ya Kesi Kufunguliwa

Kifungu cha 101 (1) (b) cha Sheria ya ya Hifadhi ya Wanyamapori [Sura ya 283 Marejeo ya 2022] kinaruhusu uteketezaji wa Nyara zinazoharibika haraka wakati wowote baada ya kesi kufunguliwa katika Mahakama yenye mamlaka ya kusikiliza shauri husika. Maombi haya yanaweza kuombwa kwa mdomo wakati wa mwenendo wa shauri na mwendesha mashtaka. Jambo la kuzingatia ni kwamba kwa amri zozote za uteketezaji vielelezo ambazo ni vielelezo katika mashauri husika, ushirikishwaji wa mtuhumiwa ni wa lazima. Hivyo, Mahakama itapaswa kutoa nafasi kwa mtuhumiwa kutoa maoni au pingamizi kabla ya kutoa amri ya kuteketeza kielelezo na kuandika kwenye kumbukumbu za mwenendo wa shauri maoni au pingamizi litakalotolewa na mshtakiwa. Vivyo hivyo, kama mshtakiwa hatasema lolote baada ya kupatiwa nafasi, kumbukumbu za mahakama zitatakiwa kuonesha hivyo. Mahakama ikikubaliana na ombi la kuteketeza kielelezo inapaswa kueleza bayana kuwa uteketezaji wa nyara husika utafanywa na Mkurugenzi wa Wanyamapori au Maafisa wengine waliokasimishwa mamlaka ya uteketezaji – Soma vifungu vya na 3, 7(1), (4) na 101(1)(a) vya Sheria.

**3. HITIMISHO**

Kama ambavyo imeelezwa hapo juu, fomu ya inventori au amri ya uteketezaji wa kielelezo kinachoharibika haraka husimama kama mbadala wa kielelezo halisi ambacho mtuhumiwa anadaiwa kukutwa nacho. Ni muhimu kuzingatia kwamba dhumuni la kuruhusu uteketezaji wa kielelezo kinachoharibika haraka ambacho hakiwezi kusubiri hadi wakati wa kusikilizwa kesi au kama kesi imeanza hadi kukamilika kwa usikilizwaji wa kesi ni kuwepo kwa uthibitisho kuwa kuliwahi kuwa na nyara au kielelezo halisi ambacho mshtakiwa anadaiwa kukutwa nacho. Mbadala wa kielelezo hicho ni inventori au amri ya Mahakama inayothibitisha kuwa nyara husika ilikuwepo, na Hakimu aliridhia iteketezwe baada ya kusikiliza pande zote mbili. Hivyo, ni muhimu inventori na amri hizi zitolewe kwa usahihi na kwa mujibu wa sheria ili ziweze kutumika kama ushahidi mahakamani.



*Aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Balozi Dkt. Pindi Chana akikata utepe kuashiria Uzinduzi wa Miongozo ya Ushughulikiaji wa Kesi za Wanyamapori na Misitu pamoja na Kesi za Uvuvi Haramu kwa Waendesha Mashtaka na Wapelelezi katika hafla ya Uzinduzi huo iliyofanyika tarehe 19 Februari, 2024.*

# Uhalifu Haulipi

**Na Adelaide Samson Kassala, Paul Aloyce Kusekwa, Tussa Jackson Mwaihesya**
**Mawakili wa Serikali**

## 1. UTANGULIZI

Uhalifu ni kitendo chochote anachotenda mtu kinyume na sheria za nchi. Katika nchi yetu uhalifu upo wa aina mbalimbali na unazuiwa au kusimamiwa na sheria tofauti tofauti ambazo zimetungwa kulingana na uhalifu huo kama vile mauaji, ujangili, wizi, ubakaji, uvuvi haramu, ugaidi n.k. Wahalifu wengi wanafanya uhalifu kwa kutumia mbinu mbalimbali na kwa kujipanga (organized crime) hivyo wakati mwingine inakuwa sio rahisi wahalifu hao kudhibitiwa na vyombo vya sheria. Wengi mtakubaliana kuwa sehemu kubwa ya uhalifu hufanywa kwa lengo kujipatia kipato au kuboresha maisha kwa wahalifu na sehemu ndogo sana ya uhalifu huwa na dhamira tofauti na ya kujipatia kipato. Katika kuhakikisha uhalifu unapungua au unaisha, Serikali kupitia Bunge imekuwa ikifanya marekebisho ya sheria mbalimbali ili kuhakikisha uhalifu unadhibitiwa na wahalifu hawanufaiki kwa namna yoyote kwa uhalifu waliotenda. Sambamba na hilo watendaji wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka pamoja na wa vyombo vya upelelezi wamekuwa wakipokea mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi ili kuweza kupambana na uhalifu ikiwa ni pamoja na kubaini mbinu mpya za kiuhalifu.

Katika kupambana na vitendo hivyo vya kiuhalifu Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ambayo inasimamiwa na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini[1] inajukumu la kushtaki na kuendesha mashauri ya jinai ambayo yanatokana na vitendo vya kiuhalifu kwa niaba ya Jamhuri na mamlaka hayo ni mamlaka ya kikatiba ambayo yameainishwa katika ibara ya 59B (1) (2) ya katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977[2].

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kutekeleza majukumu yake imejikita katika dira yake inayosema "Haki Amani na Usalama kwa maendeleo ya Taifa" lengo kuu ni kuhakikisha kila mtu anapata haki yake, uhalifu unashughulikiwa, amani inapatikana na Taifa letu linaendelea kukua katika nyanja zote. Pia uwepo wa Amani unasaidia kuboresha mazingira ya uwekezaji kwani kila mtu ataona nchi yetu ni sehemu salama ya kuhamisha na kuweka mitaji katika vyanzo mbalimbali vya uzalishaji mali.

## 2. DHANA YA MSEMO UHALIFU HAULIPI

Msemo huu una maana ya kwamba mhalifu asinufaike na kitendo chochote cha uhalifu mara atakapowekwa chini ya udhibiti wa sheria. Katika hali ya kawaida wahalifu wengi hufanya uhalifu kwa lengo la kujipatia kipato, kujijenga kiuchumi kwa njia zisizo halali na hivyo kujiwekea akiba benki, kununua mali kama nyumba, mashamba, magari na mali nyinginezo. Ofisi ya Taifa ya mashtaka katika kutekeleza majukumu yake imejiwekea mpango mkakati kuhakikisha hakuna muhalifu yeyote atakaye nufaika kutokana na kitendo chake cha uhalifu. Hii ina maana ya kwamba kitu chochote kilichotumika kutenda au kusaidia kutenda uhalifu au mali yoyote iliyopatikana kutokana na kitendo au matendo ya uhalifu (zao la uhalifu)[3] hazimnufaishi muhalifu.

1 *Sheria ya Huduma ya Mashtaka ya Taifa Sura ya 430 Rejeo ya 2019*

2 *Katiba ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania ya 1977.*

3 *Kifungu cha 9 cha Sheria ya Mazalia ya Uhalifu, Sura ya*

Ofisi inasimamia dhana hii kwa kuhakikisha mali hizo zinataifishwa na serikali pale kesi zinapofikia mwisho kwa kupeleka maombi mahakamani kwa mujibu wa sheria za nchi.

Katika dhana hii yenye nia ya kukomesha kabisa uhalifu nchini, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kwanza kabisa imeweka katika muundo wake Sehemu Maalumu ya Kutaifisha na Kurejesha Mali Zitokanazo na Uhalifu (Asset Forfeiture and Recovery Section) na imekuwa ikitekeleza zoezi la kutaifisha mali zilizotumika kufanya au zitokanazo na uhalifu kwa kushirikiana wa wadau mbalimbali wa haki jinai vikiwemo vyombo chunguzi kama vile Polisi, Uhamiaji, Mamlaka ya mapato, Bandari, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, Mamlaka za kupambana na dawa za Kulevya, Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania, Baraza la Taifa la Mazingira, Ofisi ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba n.k

*256 rejeo 2022*




**Mhalifu Yanga Omary Yanga wa Tanga**

### 3. SHERIA ZINAZOTUMIKA KUHAKIKISHA UHALIFU HAULIPI

Sheria mbalimbali zimetungwa ili kuhakikisha uhalifu haulipi, sheria hizo ni pamoja na Sheria ya Udhibiti wa Makosa ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa sura ya 200 rejeo la mwaka 2022[4], Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa sura ya 329 rejeo la mwaka 2022[5], Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai sura ya 20 rejeo la mwaka 2022[6] na sheria mama ambayo ni Sheria ya Mazalia ya Uhalifu (Proceeds of Crime Act) sura ya 256 rejeo la mwaka 2022[7] Sheria hii katika sehemu ya pili imetoa muongozo wa namna ya kutaifisha mali iliyotumika katika kutenda uhalifu au kusaidia. Vilevile, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kusimamia utaifishaji na urejeshaji wa mali zitokanazo na uhalifu imeandaa mwongozo kwa vyombo mbalimbali vya kijinai ambao unatoa namna bora ya kutambua, kuchunguza, kufungua maombi mahakamani na kuzisimamia mali zinazosubiri kutaifishwa au zilizotaifishwa ikiwa ni pamoja na kulinda thamani ya mali hizo (Asset for Forfeiture, Recovery and Management Guidelines).

### 4. UHALIFU HAULIPI MKOANI TANGA

Mkoa wa Tanga ni mkoa uliopo ukanda wa bahari ya Hindi upande wa mashariki na kupakana na nchi ya Kenya upande wa kaskazini[8] hivyo kumekuwepo na bandari bubu nyingi zenye kupitisha magendo ikiwa ni pamoja na madawa ya kulevya aina mbalimbali kinyume na sheria za nchi, hivyo makosa ya usafirishaji madawa ya kulevya yamekuwa mengi. Pia biashara hii inaaminika kuwa ni biashara inayofanywa na watu matajiri hivyo inakuwa ngumu kuwakamata.

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Tanga imekuwa ikihakikisha kwamba inatekeleza kauli

4 *Kifungu cha 23(3)(a)(b)(c) na (d), 23(4) (a) na (b)*
5 *Kifungu cha 40(1)(2) (3), kifungu 41(1) na (2)*
6 *Kifungu 351(1)(a) (b)*
7 *Kifungu cha 9(1)(a)(b)(c) na kifungu cha 14(1)(2)*
8 *https://sw.wikipedia.org/wiki/Mkoa_wa_Tanga*

mbiu ya uhalifu haulipi kwa kuratibu upelelezi wa mali zilizotumika au kusaidia katika kutenda uhalifu pamoja na mali zilizopatikana kutokana na uhalifu (zao la uhalifu). Baada ya utambuzi wa mali zilizotumika katika kutenda au kusaidia uhalifu kutendeka, mali hizo hutolewa mahakamani kama kielelezo wakati wa uendeshaji wa shauri na pindi shauri linapomalizika ikiwa mhalifu ametiwa hatiani na Mahakama, maombi hufanyika ili kutaifisha mali hiyo iliyotumika kutendea uhalifu kwa lengo la kukomesha vitendo hivyo na kuzuia mhalifu kunufaika na uhalifu aliotenda.

Kwa mali ambazo zimepatikana kama zao la uhalifu, maombi huwasilishwa mahakamani kwa ajili ya kutaifisha mali hizo ili kuhakikisha kwamba muhalifu hanufaiki na mali hizo alizozipata kupitia uhalifu, kwa mfano nyumba, gari, fedha katika akaunti za benki n.k

**YANGA OMARY YANGA CHINI YA UDHIBITI WA SHERIA: UHALIFU HAULIPI**

Mkoani Tanga kuna mtu mmoja alikuwa maarufu sana akijulikana kama “rais wa Tanga[9]” jina lake halisi ni Yanga Omari Yanga. Mtuhumiwa huyu alikamatwa na dawa za kulevya aina heroini zenye uzito wa gramu 1059 ambapo Yanga @ rais wa Tanga na wenzake Rahma Ally Juma (mke mdogo wa Yanga) na Halima Anuary Mohamed (mfanyakazi wa ndani wa Yanga Omary) walishtakiwa kwa kosa la kusafirisha dawa za kulevya aina ya Heroini[10].

Shauri hili lilisikilizwa katika Mahakama Kuu ya Tanzania, Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi ambapo ushahidi ulionesha makachero wa Mamlaka ya Kuthibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (Drug Control and Enforcement Authority) “DCEA” walikua na taarifa ya mshtakiwa wa kwanza "rais wa Tanga" kujihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevya.

Hivyo basi walianza kumfuatilia, ilipofika saa 7:30 usiku siku ya tarehe 1/10/2018 wapelelezi hao walipokea taarifa kuwa "rais wa Tanga" tayari amechukua mzigo kutoka bandari bubu na anaelekea katika nyumba yake nyingine aliyokuwa anaishi na mke mdogo Rahma Ally (mshtakiwa wa pili) iliyopo mtaa wa Bombo/ Raskazone akiwa na gari aina ya Toyota Land Cruiser lenye namba za usajiri T. 325 DJX.

Baada ya taarifa hiyo makachero hao walifika nyumbani kwa "rais wa Tanga" wakakuta gari la rais wa Tanga (“Shangingi”) likiwa limeegeshwa na wakati huo "rais wa Tanga" akiwa yupo ndani na mke wake mdogo. Alipoamshwa alitoka akiwa ameshikilia bastola, baada ya makachero kujitambulisha akiwepo mwenyekiti wa mtaa wa Raskazone, upekuzi ulifanyika katika nyumba hiyo. Katika chumba cha mfanyakazi chini ya uvungu wa kitanda ulipatikana mfuko wa rangi ya pinki ukiwa na unga na katika kabati ilipatikana mifuko mitatu ambapo mifuko miwili ilikua ya nailoni ang’avu na mfuko mmoja wa nailoni nyeusi, mifuko yote ilikuwa ya unga udhaniwao kuwa ni dawa za kulevya, na katika kabati lililokuwa koridoni karibu na chumba cha "rais wa Tanga" kilipatikana kifurushi kilichofungwa kwenye soksi nyeusi pamoja na mfuko wa nailoni nyeusi ambazo zilikuwa ya unga udhaniwa kuwa ni dawa za kulevya.

Baada ya ukamataji huo vifurushi vyote vilipelekwa maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa uchunguzi wa kisayansi ambapo ilibainika vile vifurushi viwili vilivyopatikana katika kabati karibu na chumba cha rais wa Tanga vilikuwa dawa za kulevya aina ya heroini[11]. Hivyo mahakama ilimtia hatiani rais wa Tanga na kumpa adhabu ya kutumikia kifungo cha miaka therathini, ambapo washtakiwa wenzake waliachiliwa huru.

**MBIO ZA SAKAFUNI HUISHIA UKINGONI**

"rais wa Tanga" alijaribu alikata rufaa Mahakama

9 *https://eatv.tv/sw/node/63819 Friday, 20th Nov, 2020*

10 *Republic vs Yanga s/o Omary Yanga and 2 Others (Economic Case 1 of 2020) [2020] TZHCCED 5 (20 November 2020) Tanzlii.*

11 *Republic vs Yanga s/o Omary Yanga and 2 Others (Economic Case 1 of 2020) [2020] TZHCCED 5 (20 November 2020) Tanzlii.*

ya Rufani[12] bila mafanikio kutokana na ushahidi madhubuti uliowasilishwa mahakamani dhidi yake rufaa yake ilitupwa na hivyo upande wa Jamhuri ulipata nafasi ya kutekeleza mkakati wa Uhalifu haulipi.

## 5. UTEKELEZAJI WA MPANGO MKAKATI WA UHALIFU HAULIPI

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka katika kuhakikisha jamii inapata ujumbe kuwa uhalifu wa aina yoyote haulipi au wahalifu hawawezi kuendelea kunufaika na vitu vilivyopatikana kwa njia isiyo halali, iliwasilishwa maombi ya kutaifisha mali katika Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi. Katika maombi hayo, mahakama iliombwa kutaifisha jumla ya mali 27 zikiwemo, nyumba, magari pamoja na viwanja, Mali hizo ni zile zilizopatikana kwa muda wa miaka kumi nyuma toka siku kosa alililoshitakiwa nalo kutendeka. Hata hivyo baada ya kusikiliza maombi hayo mahakama ilitoa amri ya kutaifisha viwanja saba vilivyopo maeneo mbalimbali katika jiji la Tanga ambavyo ilithibitika kuwa ni mazao ya uhalifu[13] ambayo yalipatikana ndani ya miaka kumi kabla ya "rais wa Tanga" kutenda kosa la kupatikana na dawa za kulevya na kushtakiwa.

## 6. MATOKEO CHANYA KWA JAMII YA MKOA WA TANGA BAADA YA RAIS WAO KUTIWA NYAVUNI PAMOJA NA MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO MKAKATI WA UHALIFU HAULIPI

Jamii ya mkoa wa Tanga ilipigwa na taharuki kubwa sana baada ya kuona "rais wa Tanga" amekamatwa na kuwekwa kama wahalifu wengine licha ya umaarufu wake na utajiri aliokua nao ambao kimsingi ndivyo vilivyomsababishia kupewa jina hilo la "rais wa Tanga".

Wakati Rais wa Tanga akiwa mahabusu, mahabusi wenzake walikua wakiwasihi na kuwatahadharisha ndugu jamaa na marafiki zao kuwa waache kufanya uhalifu hasa kujihusisha na dawa za kulevya kwani serikali ina mkono mrefu na haijalishi mhalifu ni mtu wa namna gani inawezekana kukamatwa kwakua wameweza kumkamata Rais wa Tanga na kumuweka mahabusu kama wao. Taarifa hizi zilienea kwa jamii ya wakazi wa Jiji la Tanga kiasi kwamba walidiriki kufika mahakamani kujihakikishia kama ni kweli raisi wao si raisi tena bali ni mahabusi.

Ofisi yetu katika kuhitimisha kesi hii ya Rais wa Tanga kutiwa hatiani na mali zake kutaifishwa. Matokeo haya yalisababisha jamii kwa ujumla kubadilika na kuogopa kujihusisha na uhalifu hasa wa dawa za kulevya kutokana na kile kilichoonekana kuwa mbio za sakafuni huishia ukingoni kwani mali zinazopatikana kwa njia za uhalifu ni sawa na nguo ya kuazima ambavyo haisitiri kwani mda wowote utakapo bainika zinataifishwa na kumuacha mhalifu kama alivyo. ***Ama kweli Uhalifu Haulipi…***

***Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai sura ya 20 rejeo la mwaka 2022[1] na sheria mama ambayo ni Sheria ya Mazalia ya Uhalifu (Proceeds of Crime Act) Sura ya 256 rejeo la mwaka 2022[2] Sheria hii katika sehemu ya pili imetoa muongozo wa namna ya kutaifisha mali iliyotumika katika kutenda uhalifu au kusaidia***

1 *Kifungu 351(1)(a) (b)*

2 *Kifungu cha 9(1)(a)(b)(c) na kifungu cha 14(1)(2)*

12 *Yanga Omari Yanga vs Republic (Criminal Appeal 102 of 2019) [2021] TZCA 220 (1 June 2021)* Tanzlii

13 *Director of Public Prosecutions vs Yanga Omary Yanga (Economic Application No.1 of 2021) [2023] TZHCCED 10 (30 June 2023)*

# Mashtaka Sports yatikisa katika michezo ya SHIMIWI na MEI MOSI

**Na Basilius Yusuf Namkambe**

**Wakili wa Serikali**

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeanzishwa kama ofisi huru ya umma kupitia Tangazo la Serikali Na.49 la tarehe 13 Februari, 2018 kwa ajili ya kutekeleza mamlaka ya kikatiba aliyopewa Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye anatoa mchango mkubwa katika kusimamia haki jinai nchini. Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2018 kwa mara ya kwanza mwaka wa fedha 2023/2024, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka imeshiriki katika mashindano ya Shirikisho la Michezo ya Wizara na Idara za Serikali (SHIMIWI) yaliyofanyika mkoani wa Iringa mwezi Octoba, 2023.

Ushiriki huu kwa namna ya pekee ulisukumwa na uongozi wa Menejimenti ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka ikiongozwa na Mkurugenzi wa Mashtaka ambaye alihakikisha kuwa wanamichezo wenye sifa wanashiriki mashindano hayo ili kuwapa fursa ya kushindana kwa faida yao na kujenga mahusiano miongoni mwao na washiriki wengine wa SHIMIWI pamoja na kuimarisha afya. Kwa muktadha huo, timu iliandaliwa bajeti ya mashindano katika hatua za maandalizi na mashindano.

Aidha, jumla ya wanamichezo 44 walishiriki katika mashindano hayo ya SHIMIWI katika michezo ya mpira wa miguu, pete, darts, kuvuta kamba, bao, kuendesha baiskeli, kurusha tufe, riadha na mbio za kupokezana vijiti.

Kati ya michezo hiyo, timu ya Mashtaka ilifanya vizuri kwenye michezo ya riadha wanaume, darts wanawake, bao wanaume na wanawake. Sambamba na matokeo hayo mazuri, pia timu ya mpira wa miguu na kuvuta Kamba zilifanikiwa kufika hatua ya robo fainali licha ya upinzani mkali kutoka timu zenye uzoefu katika mashindano haya.

Pongezi za pekee zimuendee mwanariadha wa mita 100 na 200 Bwana Majid Matitu, Wakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mkoa wa Iringa kwa kuipatia timu ya Mashtaka medali mbili. Mchezaji huyu aliibuka mshindi wa pili katika fainali ya riadha mita 100 na wa tatu katika mita 200. Pia katika mita 400 alishika nafasi ya nne.

Hii ni historia ya pekee kwa taasisi kutokana na sababu kwamba ni kwa mara ya kwanza Mashtaka Sports kushiriki katika michezo ya SHIMIWI, licha ya uchanga wake katika michezi hiyo timu zake zilitikisa timu kongwe na kuweka rekodi ya kupata medali mbili ya shaba na fedha.

Kufuatia mafanikio hayo, Mkurugenzi wa Mashtaka pamoja na menejimenti kwa kutambua mchango wa mwanariadha aliyetwaa medali hizo mbili, iliandaa hafla ya kipekee na kumtunuku zawadi siku ya mkutano wa Baraza la wafanyakazi uliofanyika jijini Mwanza mwanzoni mwa mwaka huu. Katika hafla hiyo Mkurugenzi wa Mashtaka alimkabidhi ngao pamoja na zawadi maalumu kutambua mchango wake katika timu.

Akizungumza katika tukio hilo, Mkurugenzi wa Mashtaka aliwapongeza wanamichezo

wote walioiwakilisha taasisi kwa mafanikio waliyoyapata huku akiwataka kujiandaa vema kwa ajili ya mashindano yajayo.

"..Nawapongeza kwa dhati kabisa wanamichezo na viongozi mliotuwakilisha katika mashindano yaliyoisha. Mmeitangaza vema taasisi ambayo imeshiriki kwa mara ya kwanza" alisisitiza Mkurugenzi wa Mashtaka wakati wa hafla.."

Kwa upande mwingine, Mwenyekiti wa Mashtaka Sports ameeleza kwamba timu ilishiriki katika michezo ya mei mosi kwa mafanikio makubwa. Katika michezo hiyo Mashtaka Sports iliibuka na medali tano katika riadha na medali moja katika mchezo wa draft.

Tathmini iliyofanywa imebainisha kwamba ushiriki wa timu katika michezo ya SHIMIWI na MEI MOSI umekuwa wa tija na faida mbalimbali hasa ya kulitangaza jina la taasisi yetu kwa jamii. Washiriki mbalimbali walipata nafasi ya kuijua taasisi hasa majukumu yake kupitia nafasi walizopewa viongozi wa Mashtka Sports kuzungumza na wanamichezo na vyombo vya habari. Michezo inasaidia kujenga na kuimarisha ushirikiano baina ya wafanyakazi wa Ofisi ya Taifa ya Mashtaka na wafanyakazi wa taasisi na idara nyingine za serikali pamoja.



*Mkuu wa Dawati la Jinsia na watoto Naibu Kamishna wa Polisi (DCP) Maria Nzuki kwa niaba ya Mkuu wa Jeshi la Polisi Tanzania (IGP) Camillus Wambura akimvalisha medali ya ushindi kwa mshindi wa pili (2) wa Riadha mita 100 ndg. Majid Matitu kutoka Mashtaka Sports Club ikiwa ni ishara ya kutambua juhudi zake katika mashindano hayo.*




*Mkurugenzi wa Mashtaka akiwa katika picha ya pamoja na timu ya Mashtaka Sports Club wakati wa Mashindano ya SHIMIWI yaliyofanyika mkoani Iringa mwezi Oktoba, 2023.*




*Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Bw. Sylvester Mwakitalu akisaini Kitabu cha Maombolezo kufuatia kifo cha aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Bw. Joseph Pande Jijini Dodoma tarehe 22 Desemba, 2023.*

# Msiba wa Joseph Sebastian Pande Aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Uliogeuka Kuwa Darasa la Uongozi na Utu


**Na, Ignas Mwinuka & Tulumanywa Majigo**

**Mawakili Wa Serikali.**


## Utangulizi

Ni kama mshumaa uliozima gizani ukiacha nuru ikiendelea kuangaza, hivyo ndivyo unaweza kutafsiri maisha ya aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Bw, Joseph Sebastian Pande ambapo kwa tarehe 20 Desemba, 2023 masikio ya Watumishi Ofisi Taifa ya Mashtaka yalipitia kipindi kigumu kusikia taarifa ya kuaga dunia ya Bw, Joseph Sebastiani Pande. Katika siku zilizofuatutia ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam na Dodoma ikawa zamu ya macho kushiriki katika maumivu kwa kushuhudia mwili wa mpendwa wetu ukiwa katika jeneza ukisubiri kupumzishwa katika nyumba ya milele iliyoandaliwa katika Wilaya ya Kahama Mkoani Shinyanga.

Miongoni mwa mashuhuda alikuwa ni Kasisi aliyemhudumia Kiroho katika Kanisa Katoliki lililopo eneo la Ilazo ndani ya Wilaya na Mkoa

wa Dodoma akitoa ushuhuda usio na shaka kwa kusema kwamba mpendwa wetu pale anapokuwa Dodoma alikuwa akishiriki misa za asubuhi kabla ya kuelekea kazini. Aliendelea kueleza zaidi kwamba, pasipo kujali ukubwa wa cheo chake amewahi kumuona akishika fagio na kufanya usafi kanisani huku akijichanganya na watu wengine, hivyo ilikuwa ni vigumu kujua mpendwa wetu alikuwa ni cheo kikubwa kazini kwake. Ushuhuda wa Kasisi unaendana na uhalisia jinsi alivyokuwa akiishi kwa unyenyekevu kwa Mungu na Binadamu sikuzote alitanguliza utu.

Kasisi aliendelea kusema siku za mwisho kabla ya kufikwa na mauti alimwomba nyumbani kwake, ambapo alimwambia Kasisi yupo salama kabisa rohoni mwake na akitokea amefariki basi afanyiwe Misa takatifu hapo parokiani Ilazo kabla ya kuepelekwa Kahama kwa Mazishi. Tarehe 22/12/2023 waombolezaji walikusanyika Ilazo na tarehe 23/12/2023 waombolezaji walikusanyika Kahama kutekeleza maelekezo yake aliyoyatoa kwa Kasisi.

## TAREHE 22/12/2023 PAROKIANI ILAZO

Tarehe 22/12/2023 ilifanyika ibada ya Misa Takatifu parokiani Ilazo, kanisa lilifurika umati wa watu mbalimbali wakiwemo viongozi wa kiroho, viongozi wa kutoka tasisi mbalimbali za Serikali, Mawakili wa Serikali na kujitegemea, Ndugu jamaa na rafiki wa Marehemu. Hotuba na mahubiri zilizotolewa kanisani kuhusiana na marehemu kwa hakika zilisadifu wasifu uliosomwa Kanisani kuwa mpendwa wetu alikuwa mchapakazi, mnyenyekevu, mkarimu, mwenye hekima na mwenye ubunifu.

## TAREHE 23/12/2023 KAHAMA

Umati mkubwa watu ulijitokeza Dar Es Salaam, Ilazo-Dodoma na Kahama kumuaga hii ilidhihirisha ushahidi wa wazi kuwa mpendwa wetu aligusa maisha ya watu wengi. Muwakilishi wa mwananzengo Kahama alisema kuwa mpendwa wetu alikubalika sana katika jamii yake anayoishi. Alieleza akiwa hapo usingeweza kumdhani kuwa ni mtu mwenye mamlaka katika jamii maana alieleza zaidi kuwa mtoto kwa wazazi na wazee wanaozumguka wanakiri alikuwa ni mtu mwenye maadili, heshima mbali na kuwa na elimu na mamlaka lakini havimkumfanya kujitweza. Yamkini alitambua kuwa elimu na mamlaka aliyokuwanayo amepewa bure na Mungu kwa ajili ya kuwatumikia watu wake. Hotuba na Mahubiri yaliyotolewa yaliendelea kuweka msisitizo yale yalisomwa hapo kabla kuwa mpendwa wetu alikuwa mchapakazi, mnyenyekevu, mkarimu, mwenye hekima na mwenye ubunifu. Wema hauozi ni kauli nyingine aliyothibitishwa na Mkurugenzi wa Mashtaka akiwambia watoto wa marehemu kuwa hawatatetereka kwa kuwa Baba yao amefanya mema mengi kwa watu hivyo wawe na matumaini kuwa mema aliyoyafanya Baba yao kwa watu yatawasaidia katika Maisha yao.

## MAZISHI

Mpendwa wetu alizikwa tarehe 23/12/2023 katika makazi ya Baba yake mzazi aitwaye Sebastian Pande huko Kahama. Ni dhahiri tunatembea juu ya udongo, tunalima juu udongo, tunajenga juu ya udongo na tunafanya shughuli zote juu ya udongo kumbe siku ya siku ni udongo unaofaidika kwa kutuchukua kuwa sehemu yake kwa mpendwa wetu udongo utafanikiwa kuchukua mwili wake lakini hautafanikiwa kuchukua ukarimu, upendo, unyenyekevu, hekima, uchapakazi kwani matendo mema ya mpendwa wetu yanaishi ndani mwetu.

***"Hakika tutaishi mema yako, pumzika kwa amani"***




*Mkurugenzi wa Mashtaka nchini Bw. Sylvester Mwakitalu akiweka mashada ya maua kwenye kaburi la Marehemu Joseph Pande mara baada ya kushiriki kwenye ibada ya mazishi iliyofanyika tarehe 23 Desemba, 2023 katika Kanisa la Parokia ya Mtakatifu Stephano Shahidi, Nyasubi lililopo Wilaya ya Kahama katika Mkoa wa Shinyanga.*



*Mawakili wa Serikali kutoka Ofisi ya Taifa ya Mashtaka wakiwa wamebeba mwili wa aliyekuwa Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka Sebastian Joseph Pande kuelekea kanisani*

# Utani wa Kisheria

Na Tawabu Yahya Issa
Wakili wa Serikali

## Kesi ya Trafiki Meatu

Dereva mmoja aliendesha gari kwa uzembe na kusababisha ajali, alivyofikishwa mahakamani wakati wa utetezi wake akasema kuwa wakati anaendesha gari hilo ghafla aliona punda mbele yake lakini alivyoshika breki, gari lilipoteza breki hivyo ikapelekea yeye kugonga kingo za daraja na kupata ajali. Wakati wa maswali ya dodoso akaulizwa, kuwa je na kawaida gari lako huwa likiona punda linapoteza breki? akajibu hapana, alivyoulizwa kwanini hiyo siku alivyoona punda breki zikapotea? Hakuwa na la kujibu… jamaa alitiwa hatiani kwa kuendesha gari kwa uzembe na kuhukumiwa kulipa faini ya shilingi 50,000/-

Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Makao Makuu, S.L.P 1733 Dodoma.

## Anuani za Ofisi ya Taifa ya Mashtaka Mikoa

| | | |
|---|---|---|
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 14370<br>Dar es salaam | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 997<br>Songea - Ruvuma | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 6066<br>Morogoro |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 331<br>Mwanza | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 992<br>Bukoba | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 30393<br>Pwani |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S. L.P 3144<br>Arusha | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 321<br>Sumbawanga - Rukwa | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 587<br>Geita |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 199<br>Tabora | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 2401<br>Iringa | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 131<br>Mpanda - Katavi |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 963<br>Dodoma | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 635<br>Shinyanga | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 169<br>Bariadi - Simiyu |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 6433<br>Moshi | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 1073<br>Lindi | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 362<br>Vwawa - Songwe |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 970<br>Mbeya | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 823<br>Musoma - Mara | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 324<br>Tarime |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 418<br>Tanga | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 44<br>Singida | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 39806<br>Temeke |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 174<br>Mtwara | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 498<br>Kigoma | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 6240<br>Ilala |
| Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 165<br>Njombe | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 295<br>Babati - Manyara | Ofisi ya Taifa ya Mashtaka<br>S.L.P 75601<br>Kinondoni |